



UPINZANI HAUJAISHA-

Miaka 500 baada ya Luther



UPINZANI HAUJAISHA -

Miaka 500 baada ya Luther

Mnamo Oktoba 31, 2017, ilikuwa miaka 500 tangu Martin Luther alipogongomelea hoja 95 kwenye mlango wa kanisa huko Wittenberg. Hoja hizi 95 kanisa zilifichua baadhi ya mapokeo na mafundisho ya Kanisa Katoliki yasiyokuwa ya Biblia. Watu wanashangazwa sana kwamba mtu mmoja angeweza kuthubutu kufanya jambo kama hilo. Hebu fikiria kuzungumza na kuipinga Rumi—mtu mmoja dhidi ya mfumo mzima.

Hoja 95 zilienezwa kote Ujerumani na sehemu zingine zote za ulimwengu katika kipindi kifupi sana. Watu walielewa

haraka kwamba Kanisa Katoliki lilihimiza mafundisho na mapokeo potofu, na hivyo likaingia kundi la Luther. Midahalo mingi makini ilitokea na hoja hizi 95 ziliwafanya watu wafikirie kwa namna tofauti kwa ajili yao wenywewe.

Makasisi pekee ndio waliokuwa na Biblia; walitegemewa na watu. Walitumainiwa kuwasilisha neno la Mungu kwa usahihi. Martin Luther, pamoja na hoja zake 95 na mahubiri, alidhihirisha kwamba mapokeo na mafundisho ya makasisi hayakupatana na mafundisho ya Biblia. Hapo yakatokea haraka makundi mawili tofauti ya watu—



Luther mbele ya Baraza la Worms, April 1521.

Kanisa Katoliki dhidi ya mafundisho ya Luther. Kwa vile Luther alidumisha mafundisho yake na kwa mafundisho yake haya, hatimaye aliiwa mbele ya Baraza la Worms. Baraza hili lilimtaka akubaliane desturi za wakati huo na kukana yote aliyokuwa amesema na kufanya. Hata hivyo, Luther alisema: “*Thibitisheni kutoka kwenye maandishi ya manabii na mitume kwamba nimekosea. Mara nitakaposhawishika juu ya hili, nitakana kila kosa, nami nitakuwa wa kwanza kushika vitabu vyangu na kuvitupa motoni.*” Aliendelea, “*Siwezi kusalimisha imani yangu ama kwa papa au mabaraza, kwa sababu ni dhahiri kama ilivyo mchana kwamba wamekosea mara nyangi na kujikanganya wenyewe. Isipokuwa kama nikishawishiwa kwa ushuhuda wa Maandiko au kwa mantiki wazi kabisa, isipokuwa kama nikishawishiwa kwa njia ya maandikoya Biblia ambayo nimenukuu, na isipokuwa yakifanya dhamiri yangu ifungwe kwa neno la Mungu, siwezi na wala sitakana, kwa vile si silama kwa Mkristo kuzungumza kinyume na dhamiri yake. Uamuzi wangu ndio huu, siwezi kufanya lingine lolote; Mungu aweze kunisaidia. Amina.*” (D’Aubigné, kitabu cha 7, sura ya 8)

Upinzani wa viongozi wakuu Wakristo

Mfalme Charles V alitaka kumzuia Luther pamoa na kukomesha Matengenezo. Alitisha Baraza la Spires mnamo mwaka 1529, akiwapendeza sana watu wa papa. Hapa iliamuliwa kuwazuia Wanamatengenezo wasieneze mafundisho yao. Iliamuliwa zaidi kwamba Wanamatengenezo hawakupaswa kuingia kwenye mgogoro wala kupingana na hadhara, na kwamba asiwepo Mkatoliki

hata mmoja atakayeruhusiwa kupokea mafundisho ya Luther. .

Viongozi Wakristo, walioafikiana na Matengenezo, waliamua kudhihirisha upinzani wao mbele ya baraza la kitaifa.



Kasri ya Wartburg, ngome ya mlimani mahali ambapo mwanamatengenezo huyu aliandikia vijizuu vingi viliviyosambazwa katika Ujerumanu yote na kufasiri Agano Jipyä katika lugha ya Kijerumani..

Waliandika, mionganini mwa mambo mengi: “*Hatuafiki wala hatufuati kwa namna yoyote ile agizo lilopendekezwa, kwa lolote liliolo kinyume na Mungu, kwa neno Lake takatifu, kwa dhamiri zetu sahihi, kwa wokovu wa roho zetu... Tumeamua, kwa neema ya Mungu, kudumisha mafundisho safi na pekee ya neno Lake takatifu, kama lilivyo katika vitabu nya Biblia nya Agano la Kale na Jipyä, bila kuongeza chochote humo kinachowenza kutofautiana nalo.*” (D’Aubigne, kitabu cha 13, sura ya 6).

Upinzani wao ukalipatia kanisa la matengenezo jina Protestant; kanuni zake ni msingi hasa wa Uprotestant.

Kwa Mamlaka Gani?

Martin Luther na Wanamatengenezo walidumisha mtazamo kwamba Wakristo wangepaswa kuifuata Biblia na Biblia pekee, wakati wakijadili masuala ya imani na mafundisho. Kanisa Katoliki, kwa upande mwininge, lilisema kwamba mtu angepaswa kuifuata Biblia **na** mafundisho ya kanisa. Katika wazo hili, uvunjaji ulikuwa dhahiri kabisa

Kanisa Katoliki lilisema kwamba Luther na Wanamatengenezo wangepaswa kuifuata mahitimisho ya kanisa na taifa. Wanamatengenezo walisema wangefanya hivyo tu kama mahitimisho yao haya-kuwa yakipingana na neno la Mungu. Wanamatengenezo waliamini kwamba walikuwa na haki ya kufuata dhamiri zao pale wanaposhughulika na imani na mafundisho. Rumi, kwa upande mwininge, iliamini kwamba pale wengi katika baraza la kanisa wanapokuwa wameamua juu ya jambo lililo sahihi, wote wangepaswa kufuata uamuzi wao. Matokeo yake, kila mtu alipaswa kuchukua uamuzi: ama neno la Mungu, au mafundisho ya kanisa (mapokeo) pamoja na Biblia.

Mateso

Kwa sababu Wanamatengenezo wasinge-weza kuisujidia Rumi, Kanisa Katoliki likaanza kuwatesa. Wanamatengenezo walikuwa wamepingana na mamlaka ya Rumi na sasa wangepaswa kufutiliwa mbali. Wengi mionganoni mwa Wanamatengenezo walitupwa gerezani katika mazingira ya kikatili, wengine waliteswa katika maeneo pweke ya Alps, wengine waliachiliwa wanyama wakali, wengine wengi waliteswa na Mamlaka ya Kikasisi, wakati wengine wakifa kwa upanga. Visa juu ya mateso na adhabu ya kikatili ya Kanisa Katoliki

yalitikisa ulimwengu kabla na baada ya wakati wa Luther. Wengi mionganoni mwa Wanamatengenezo walipokea vitisho na kupigwa marufuku na papa. Baada ya kupigwa marufuku na papa, yejote angeweza kuwaua. Wengi mionganoni mwa Wanamatengenezo walichomwa moto iliali wamefungwa kwenye nguzo—kama ilivyokuwa kwa Hieronymus, Jan Hus, Louis de Berquin, William Tyndale na wengine wengi. Mwili wa John Wycliffe ulifukuliwa na mifupa yake kuteketezwa kwa moto na majivu yake kumwagwa mtoni karibu na mahali hapo. Huko Uingereza pekee, palikuwa na Waprotestanti 289 waliochomwa moto kwenye nguzo wakati wa utawala wa Mary I Malkia Mkatoliki kuanzia mwaka 1555-1558. Pamoja na hili, inafaa kuona kile alicho sema Yesu: **“Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu wadio wadogo, mlinitendea mimi.”** (Mathayo 25:40). Kanisa Katoliki na viongozi wake wana mambo mengi ambayo kwayo watawajibishwa! Kwa bahati njema, Mungu ndiye atashughulikia jambo hili. Anaona mambo yote Naye atahukumu kwa haki. Ni jambo zuri kufikiria hili katika uhusiano na andiko hili: **“Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya.”** (Mhubiri 12:14).

Ni bayana kwamba kuna msamaha kwa ajili ya dhambi zote, endapo mtu husika akitubu, akiungama dhambi yake na kuomba msamaha, lakini kamwe hatujawahi kusoma au kusikia juu ya Kanisa Katoliki likienda chini ya msalaba, likiungama mateso yote ya kutisha, ukatili na mauaji ya watu waliokuwa na imani tofauti hapo kabla, wakati na baada ya siku za Luther.

Fikiria hilo. Kanisa Katoliki liliamuru mauaji ya watu kwa vile tu walikuwa na imani tofauti? Fikiria **jinsi** watu walivyo-

pitia mateso ya kutisha yaliyofanywa na Mamlaka ya Kikasisi—kwa sababu tu walikuwa na imani tofauti? Zingatia wale waliokufa kwa upanga—kwa sababu tu walikuwa na imani tofauti? Fikiria wale waliofukuzwa kwenda uhamishoni, wakapigwa marufuku katika jamii—kwa sababu tu walikuwa na imani tofauti; na orodha hii inaweza kuendelea zaidi na zaidi. Wakati huohuo, mfumo huu wa kanisa ungepaswa kutazamwa kama jumuiya ya Kikristo. Hivi tabia ya namna hiyo inahusiana kwa vyovyyote na Kristo? Hapana, si kitu kingine isipokuwa Ibilisi na Shetani aliye nyuma ya matendo hayo ya kutisha. Haikuwa siku moja tu, au mwezi mmoja au mwaka mmoja ambapo matukio haya ya kutisha yalifanyika, bali yalichukua mamia kadhaa ya miaka. Pia ni vyema kujulikana kwamba papa Benedict wa XVI aliyeppita alikuwa kiongozi wa Mamlaka ya Kikasisi hadi mwaka 2005. Leo, Mamlaka ya Kikasisi yana jina jipya—Jumuia ya Mafundisho ya Imani. Kiongozi wa sasa wa Jumuia hii ni Askofu Mkuu Gerhard Ludwig Müller.

Wanamatengenezo walitoa kila kitu kwa ajili ya kazi ya Mungu. Hata wakichomwa walimshuhudia Yesu. Habari gani sisi: Je, tunatambua kile ambacho Yesu ametufanya? Je, tunatambua upendo na neema Yake kuu kwa ajili yetu? Je, tunatoa vyote kwa ajili ya Mungu?

Wapende maadui zako

Kama tukimlinganisha Yesu na upapa, ambao umewasakama watu wa imani nyingine, Yeye anasema: ***"Lakini mimi nawaaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi."*** (Mathayo 5:44).

Hii ni roho tofauti jinsi ukilinganisha na ile ya upapa! Mungu ametuumba na kutupatia utashi ili kila mtu aweze kufanya maamuzi binafsi kuhusiana na masuala

ya kidini. Hatupaswi kuwalazimisha watu waamini kama ninavyoamini au kama uaminivyo. Wote wanapaswa kuwa na haki ya kumwabudu Mungu kulingana na dhamiri yao. Ni makosa pale ambapo kifungo magerezani, mateso na upanga vinapotumika kuwashurutisha watu



Picha Korea.net (Wikimedia Commons)

watii. Ipo tofauti kubwa kuwaua maadui na kuwapenda! Watoto wa Mungu watawapenda maadui zao. Yesu, Muumbaji na Mtegemezaji wetu, huwapenda wote (Yohana 1:3; Wakolosai 1:17). Yesu



Makao ya papa huko Vatikani

anasema: “*Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenyewe kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.*” (Mathayo 11:28). Anasema pia: “*Wote anipao Baba watakuja kwangu; wala ye yote ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe.*” (Yohana 6:37). Yesu anatamani kwamba sote tuweze kufikia hatua ya kuilewa kweli na kuokolewa.

Yesu anatamani kwamba sote tuweze kufikia hatua ya kuilewa kweli na kuokolewa.?

Papa hujihesabu kama mwakilishi wa Kristo duniani, lakini wote wanapaswa kuona kwamba mapapa hawamwakilishi Kristo. Mapapa wamejizungushia maonesho ya kifahari, lakini Yesu alisema: “*Mbweha wana pango, na ndege wa angani wana viota; lakini Mwana wa Adamu hana pa kulaza kichwa chake.*” (Mathayo 8:20). Yesu alivaa mavazi rahisi wakati ambapo mapapa wana mavazi mengi makubwa na

aghali. Mapapa huishi katika majengo ya anasa, hutumia mamilioni katika ziara na wana walinzi kila upande. Tunaona vyema kwamba papa ana mtazamo mwингine tofauti na Yesu. Kwa hiyo wadhifa ambao Kanisa Katoliki limemwekea papa haupatani kabisa! Ni dhihaka dhidi ya Kristo na maisha ya uadilifu na unyenyekevu aliyoishi.

Kanisa Katoliki lina utajiri mkubwa kupita kiasi. Yesu alimwambia yule tajiri: “*Umepungukiwa na neno moja. Enenda, ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate.*” (Marko 10:21).

Kwa vile Vitakani ina utajiri mwингi kiasi hicho, papa naye anapaswa kufuata wito huu, kama anadai kuwa mwakilishi wa Mwokozi aliye mnyenyekevu.

Martin Luther alilijua Kanisa Katoliki kutoka ndani na alisema: “*Ni jambo la kutisha sana kumwona mtu anayedai kuwa mwakilishi wa Kristo, akidhahirisha ufahari asioweza kuufikia mfalme yeote. Je, hivi ndivyo kuwa kama Yesu aliye kuwa maskini, au Petro mwenye maisha ya chini? Wao wanasema kwamba yeeye ni bwana wa ulmwengu! Lakini Kristo, ambaye papa hudai kuwa mwakilishi wake, amesema, ‘Ufalme wangu si wa ulmwengu huu.’ Hivi utawala wa mwakilishi unaweza kuwa mkubwa zaidi kuliko ule wa mkuu wake?*” D’Aubigne, kitabu cha 6, sura ya 3).

Utawala wa Kilimwengu

Wengi huamini kwamba Kanisa Katoliki limebadilika tangu lilipotenda matukio ya kikatili wakati ule wa Matengenezo—lakini halijabadilika. Lina imani na mafundisho yaleyale ambayo limekuwa

nayo wakati wote. Limejivika tu mavazi ya Kikristo ili liweze kukubalika. Sasa kwa vile limekubalika na kupokea utawala tena, si tu katika Umoja wa Ulaya, bali ulimwengu mzima, hivi punde tunaona upapa unasimama kwa ajili ya nini. Kama ambavyo ulitumia mamlaka ya nchi wakati wa Wanamatengenezo, litatumia sheria za nchi na za kimataifa ili kusaidia kujipatia utawala katika wakati wetu.

Papa Paulo wa VI aliandika mada yenyekichwa kisemacho: *Kuelekea Mamlaka Thabiti ya Ulimwengu: "Ushirikiano huu wa kimataifa ulio katika kiwango cha ulimwengu mzima huhitaji taasisi zitakazoandaa,zitakazoratibu,nakuongoza hadi hatimaye kutakapoanzisha mfumo wa haki utambulikao kilimwengu. Nani asiyeona umuhimu wa kuanzisha hivyo kwa mwendelezo mamlaka ya kilimwengu yanayoweza kutenda kwa usanisi katika sekta za kimahakama na kisiasa."* – Pope Paul VI Popolorum Progressio 1967,78.

Ndipo swali linaibuka: Ni taasisi zipi ambazo Kanisa Katoliki hushirikiana nazo, ili kuanzisha mfumo mpya wa kilimwengu? Nadhani sote tunaweza kuziona, kupitia Umoja wa Mataifa, Umoja wa Ulaya, NATO, Umoja wa Afrika, Shirika la Fedha, na kadhalika.

Papa Benedict wa XVI alitoa wito wa dhati kwa viongozi wa ulimwengu katika waraka wake wa hivi karibuni, akisema: *“Lipo hitaji la haraka la mamlaka halisi ya ulimwengu wa kisiasa, ili kusimamia uchumi wa ulimwengu unaofuata madili yaliyojengwa katika Mungu... ili kukomesha hali ya sasa ya tatizo la kifedha ulimwenguni.”* - by Cathy Lynn Grossman, USA Today, 7/7/2009.

Hatupaswi kusahau kwamba Kanisa Katoliki hutamani kuwa mamlaka ya

kilimwengu. Linatamani kuwa na utawala wa ulimwengu wote. Wakatoliki ndio walioanzisha Umoja wa Ulaya na Vatikani ndiyo iliyo nyuma ya wazo la Mfumo Mpya wa Ulimwengu. Sheria za kimataifa ndizo zitakazotawala katika Mfumo Mpya wa Ulimwengu na kwa namna hiyo kujipatia mamlaka—mamlaka ya ulimwengu.

Katika kitabu chake kilichouzika zaidi *The Keys of This Blood*, Profesa Mjesuti na mshirika wa ndani wa Vatikani, Malachi Martin, alifunua vote:

"Ama tunapenda au la, ama tuko tayari au la, sisi sote tunahusika katika ushindani wa kilimwengu wa dhati, usio na mipaka na wa namna tatu.... Sisi ni wadau.... ushindani huu unahusu



nani atakayeanzisha mfumo mmoja wa ulimwengu wa kwanza wa serikali ambayo imewahi kuwepo katika jamii ya mataifa. Ni juu ya nani atakayeshikilia na kutoa uwezo wa aina mbili wa MAMILAKA NA UTAWALA JUU YA KILA MMOJA WETU PAMOJA KAMA JUMUIA... katika milenia ya tatu... sasa kwa vile tavarishe umeanzishwa,

hakuna namna yoyote ambapo unaweza kusitishwa... mtindo wetu wa maisha kama watu binafsi na kama raia... hata nembo za utambulisho wetu... vitakuwa vimebadilisha milele kwa kiasi kubwa sana. Hakuna mtu anayeweza kuepuka athari zake. Hakuna nyanja ya maisha yetu ambayo haitaguswa.” [Msisitizo umeongezwa] - Malachi Martin, *Keys of This Blood: Pope John Paul II Versus Russia and the West for Control of the New World Order* (1991), uk. 12-16).

Martin anasema kwamba Papa atakuwa “mshindi katika ushindani huo.” Katika ukurasa wa 341 wa kitabu chake, Malachi Martin anaelea wazi kwamba serikali hii moja ya ulimwengu “itatawaliwa na urasimu wa kimataifa unaodhibiti na kumwongoza kila raia na kila taifa...

Hebu tuangalie nukuu chache zinazo-eleza jinsi Kanisa Katoliki linavyo-jitambulisha:

“Kanisa la Rumi ni himaya moja iliyo juu ya falme zote, kama ilivyo akili na mwili, au kama alivyo Mungu ulimwenguni. Kwa hiyo, Kanisa la Rumi halipaswi tu kuwa na mamlaka ya kiroho, bali pia mamlaka ya ukuu duniani.” (Pope Leo XIII, Apostolic Letter, 1879). Papa Gregory alirudia tena mtazamo huu, aliposema, “**Mamlaka ya Kanisa yako juu kuliko mamlaka ya taifa.**”

Dkt. G. F. van Schulte, profesa wa sheria

ya kikanoni, anasema: ““**Mamlaka yote ya kibinadamu hutokana na mwovu na hivyo hayana budi kudumu chini ya Papa.**” (T. W. Callaway: *Romanism vs. Americanism*, uk. 120).

Marejeo haya huweka wazi kabisa kwamba kanisa hili la kisiasa linajitahidi kupata mamlaka ya kutawala serikali na mamlaka za nchi. Kanisa Katoliki hutenda kazi kwa kuzingatia dhana ya “de jure divino,” kirai cha Kilatini chenye maana kwamba kanisa lina mamlaka matakatifu ya kutawala ulimwengu wote, milki, na watu. Hudai kuwa lilipokea haki hii kutoka kwa Mungu Mwenyewe na litatumia njia zote ili kutimiza lengo hili—utawala wa ulimwengu.

Dkt. Brorson, bingwa mashuhuri wa Kikatoliki, aliwahi kuandika: “**Papa anayo haki ya kutamka hukumu ya uondoshaji dhidi ya mtawala yeoyote, pale inapohitajika kwa maslahi ya mfumo wa kiroho... mamlaka ya kanisa yaliyotekelizwa juu ya watawala katika Zama za Kati hayakuwa unyang’aji, hayakutokana na maafikiano ya wakuu au ridhaa ya watu, bali yalidumishwa na yanaendelea kudumishwa kwa haki ya kiungu, na yule anayeyapinga, anaasi dhidi ya Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.**” (*Catholic Review*, Juni 1851).

Ingawa hii iliandikwa muda mrefu uliopita, Kanisa la Rumi linasema kwamba kamwe



Kusudi la harakati za umoja wa makanisa—kuunganisha dini zote..

halibadiliki. Dkt. Alithibitisha msimamo huu: ***"Kile ambacho Kanisa limefanya, kile ambacho limeeleza au kuidhinisha bila kusema huko zamani, ndicho hasa litakachofanya, litakachotamka au kuidhinisha bila kusema katika wakati ujao, endapo mazingira yaleyale yatajitokeza."*** (Catholic Review, Januari 1854).

Tutaona kwamba aina zote za uasi dhidi ya utawala huu katika nyakati hizi za mwisho, pamoja na kukosa kutambua mamlaka ya kanisa, zitaadhibiwa, na Umoja wa Ulaya pia.

Kabla ya Baraza la Pili la Vatikani (1962-1965), Kanisa Katoliki liliwaita wazushi watu wa imani zingine. Tangu Baraza hili, wazushi sasa wanahesabiwa kama ndugu waliojitetenga. Kanisa Katoliki husema ndilo pekee lenye kweli na kwamba hakuna wokovu nje ya kanisa lao.

Harakati za umoja wa makanisa

Kanisa Katoliki leo linajaribu kuunganisha madhehebu yote ya kanisa kuptitia harakati za umoja wa makanisa. Wamewaomba Majesuiti huko Rumi waanzishe mjadala katika madhehebu ya kanisa katika kujaribu kuwakusanya chini ya utawala wa Kanisa Katoliki. Tunaweza kuona kwamba kumekuwepo na badiliko. Kanisa Katoliki halijabadilisha mafundisho yake, bali Uprotestanti ndio umeisogelea sana Rumi.

Charta Oecumenica ni jina la waraka teule wanaotumia katika haraka za umoja wa makanisa na ni dhahiri kutoekana na waraka huu kwamba wana shauku ya kutenda kazi na kufanya kazi ya kimishenari pamoja. Wanatafuta umoja katika mambo yale

wanayoweza kukubaliana na mambo yale wasiyokubaliana kwayo huyaweka pembeni. Yesu Kristo anatamani kwamba tufkie umoja katika Yeye kwenye ngazi zote. Si umoja uliojengwa katika demokrasia na kura ya wengi, bali umoja katika Kristo. Umoja katika imani ya Yesu – katika nyanja zote. Kama hatuwezi kuwa wamoja na mabaraza ya kanisa, basi lazima tumfuate Kristo.

Wale wanaofanya kazi ya utume, bila kuingiliwa na dhehebu la kanisa, hutazamwa kama wakengeufu au aina ya wasaliti—na wasaliti hawana budi



Madona akiwa na Mtoto, kinyago kilichojaa alama za Kikatoliki. Mkono wa Kristo vidole vitatu vikiwa vimeinuliwa, kwa vile angekuwa mkatoliki. Ana tufe mkono mwake, na msalaba wa kikatoliki juu ya tufe. Huoneka kwamba Kristo anashirikiana na Kanisa Katoliki ili kutawala ulimwengu wote pamoja nao..

kushughulikiwa. Luther, Melanchton, Tyndale, Calvin, Wycliffe, Hieronymus, Wesley, Hus, Zwingli, Berquin, Waldensia



Sehemu ya dirisha lililochorwa picha katika kasri ya Loyola, Hispania. Uidhinishaji wa Jesuti ulifanyanya na Paul III katika 1540 Roma.

na wengine walihesabiwa kuwa wasaliti. "Wasaliti" hawa walitamani kuwa na Biblia na Biblia pekee kama msingi wa imanii yao. Kama ambavyo tumeona, Kanisa Katoliki lilikusudia kuzuia na kufutilia mbali waasi (Wanamatengenezo) wakati wa Zama za Giza. Wasaliti leo, Wanamatengenezo wa leo, wanapinga harakati za umoja wa makanisa. Harakati za umoja wa makanisa leo hutaka Biblia na mapokeo viwe kanuni, wakati ambapo Wanamatengenezo wa leo wanaendelea katika njia ya Luther na Wanamatengenezo wa kati wake, wakiwa na Biblia na Biblia pekee kama msingi wa imani na mafundisho.

Biblia inatamka wazi kabisa kwamba utawala huu unaotesa ungepata jeraha la mauti na kwamba jeraha hilo lingepona. Upapa ulipata jeraha la mauti mnamo mwaka 1798, wakati Papa Pius wa VI alipochukuliwa utumwani na Jenerali Berthier wa jeshi la Napoleon na baadaye

akafa kama mfungwa huko Ufaransa. Upapa ulipokea tena jimbo la Vatikani mnamo mwaka 1929 kuitia Mussolini na kuanzia wakati huo umejjipatia mamlaka na ushawishi mkubwa zaidi ulimwenguni. Papa Yohana Paulo wa II alisafiri ulimwenguni na kuanzisha mfungamano wa kidiplomasia na nchi moja baada ya nyingine. Papa Benedict wa XVI aliendelea kazi hii, na sasa Mjesuti mpya, Papa Francis, anaendelea kukusanya maeneo yote ya ulimwengu chini ya bendera ya upapa kuitia harakati za umoja wa makanisa, katika kujaribu kuleta umoja na wale waliokuwa wamejitenga. Ili kutekeleza hili, wanatunga sheria za kimataifa—sheria za kisiasa, kidini na kiuchumi/kifedha. Sheria za kimataifa zinapaswa kuwa juu ya sheria za kitaifa/mahalia na jambo hili ndilo litawawezesha kushawishi mataifa na watu. Sheria hutawala mataifa na pale taifa fulani linapokuwa chini ya sheria za kimataifa zinazotungwa na watu wa ulimwengu mzima, wanaofanya kazi kwa ajili ya kutekeleza Mfumo Mpya wa Ulimwengu, basi taifa hilo husalimisha uhuru na mamlaka yake. Maendeleo haya hufanyika katika nyanja ya kisiasa, kidini na kiuchumi/kifedha. Ni mkakati unaofanyika taratibu kwa kipindi cha miaka mingi—ni maendeleo yanayofanyika taratibu bila kutambulika. Hatimaye wale wasio waaminifu katika sheria za kimataifa, ama ni sheria za nchi au kanisa, watatazamwa kama raia wakaidi. Watakabiliwa na adhabu na aina zingine za nidhamu. Kitendo cha upapa kutumia vibaya madaraka kitashuhudiwa tena, lakini mshangao mkubwa utakuwa kwamba wale ambao hapo awali waliopinga utumiaji mbaya wa mamlaka watakuwa washirika wao (Ufunuo 13:11-17). Biblia ndiyo inayofunua jambo hili nasi tunaamini kuwa ni neno la Mungu.

Kamwe Rumi haibadiliki

Je, inakushangaza kwamba Waprotestanti sasa wananyoosha mkono wao kuelekea Rumi na wanafanya kazi pamoja na Rumi? Ni dhahiri kwamba Waprotestanti wamesahau jinsi Rumi ilivyowatesa wale wa imani zingine kama ilivyokuwa katika wakati wa Luther. Kama ambavyo tumeona, wapo wengi waliofungwa gerezani, walioteswa na kutendewa unyama kwa sababu ya imani yao. Kwa hiyo ikiwa hatujui historia yetu au Biblia yetu, hatutajua kitakachotokea katika wakati ujao. Rumi haibadiliki kamwe na historia hujirudia. Kanisa Katoliki limejivika tu mavazi ya Ukristo. Mfumo huu leo ni mbwamwitu katika vazi la kondoo. Hutenda kazi kwa kutumia papa mweupe na mweusi. Papa mweupe huvutia umati wa watu kwa ufahari na utajiri wake wote, wakati ambapo papa mwingine, kiongozi wa Majesuti, hutenda kazi kwa siri, gizani. Majesuti ndio askari wa Rumi waliofunzwa kwa siri. Kulingana na kiapo cha Jesuti, wataanzisha vita ili kuangusha serikali na hivyo kufanya utawala ukubaliane na wao. Wanahimizwa kujipenyeza katika madhehebu mengine na kuwa Mlutheri mionganoni mwa Walutheri, Mbatiisti mionganoni mwa Wabaptisti, Mpentekoste mionganoni mwa Wapentekoste, Mwadventista mionganoni mwa Waadventista, nk. Kupitia elimu wanaweza kujipatia nyadhifa na kupitia nyadhifa hizi wanaweza kushawishi kwamba dhehebu hilo lishiriki katika harakati za umoja wa makanisa. Ni waaminifu kabisa kwa papa na kama wanapenda na kama ni muhimu, wanatumia makali ya upanga au aina nytingine yoyote ya silaha ili kutimiza lengo lao. Wale wanaosoma kiapo cha Jesuti, ambacho wanakitamka kwa papa kabla hawajaanza jukumu lao, wataelewa hili. (Angalia www.endtime.net - The Elite Tightens the Grip). Waprotestanti wengi hufumbia macho mikakati ya hila ya Rumi ili kutafuta umoja katika ulimwengu wa kidini.

MAPINDUZI - Miaka 500 baada ya Luther! Kuusherehekeea Umoja—Simo Luther

Mnamo mwaka 1617, 1717, 1817, 1917 Waprotestanti walisherehekeea upinzani wa Luther dhidi ya Kanisa Katoliki, lakini mnamo mwaka 2017 hili libadilishwa. Kisha waliashiria sikuhiyo pamoja na Kanisa Katoliki huko Rumi. Hawakumsherehekeea Martin Luther na Uprotestanti, bali umoja wao na Kanisa Katoliki. Hili ni badiliko kuu kiasi gani, ni mapinduzi yalioje!

Mwaka 1999 Kanisa Katoliki lilichapisha Tamko la Pamoja na Shirikisho la Walutheri Ulimwenguni (makanisa ya Kilutheri) kuhusiana na fundisho la Haki kwa Imani, na hivyo wanatangaza kwamba upinzani umekwisha! Hata hivyo, upinzani haujaisha. Kwa neema ya Mungu upinzani huo utaendelea hadi kufungwa kwa rehema!

Mwaka 2013 kitabu kipyta kilichapishwa kiitwacho ‘From Conflict to Communion’, taarifa ya Tume ya Walutheri na Wakatoliki juu ya Umoja. Katika dondoo ya 229 katika kitabu hicho husomeka: “Ingawa wao (wanateolojia wa Kilutheri) hukubaliana kwa sehemu na ukoaji wa Luther dhidi ya upapa, hata hivyo Walutheri leo wanakataa hatua ya Luther kumtambua papa kama Mpinga-Kristo.” Hivyo leo wengi sana mionganoni mwa viongozi wa kanisa hawadhani kwamba papa ni Mpinga-Kristo. Sasa huchukulia kwamba madhehebu yote ya kanisa yanayoshiriki katika harakati za umoja wa makanisa—ikiwa ni pamoja na Papa Francis Mjesuti na Kanisa Katoliki—ni Wakristo, bila Kanisa Katoliki kubadili mafundisho yake. Kwa vile Kanisa Katoliki halijabadilisha mafundisho yake, nani basi, ambaye amebadilika, kiasi kwamba sasa wanahitaji umoja?



Sherehe ya Katoliki ya Ekaristi

Mnamo Oktoba 31, 2017 viongozi wa Walutheri na Wakatoliki hawakwenda Wittenberg, bali walikutana “kwa siri” huko Rumi. Walianda Tamko la Pamoja wakati wa kuhitimisha mwaka wa kumbukumbu ya pamoja ya Matengenezo.

Katika mchakato wa umoja wa makanisa, ni jambo la kutisha mno, lakini la kweli, kwamba Waprotestanti wamekengeuka kuelekea Rumi. Inaonekana kama vile Kanisa Katoliki limepata ngome katika madhehebu mengi, na kwamba upkee wa makanisa ya Kiprotestanti yanaangushwa taratibu. Hakuna viongozi wa dini wanaoendelea kupinga tena, sauti zote zimekaa kimya. Nani, basi, atakayepaza sauti ya upinzani? Naam, tunatumaini kwamba mimi na wewe tutafanya hivyo, bila kujali wadhifa au mvuto wetu!

Kuanzia mwaka 1999, Kanisa Katoliki limeandika kauli za pamoja na Baraza la Umethodisti Ulimwenguni, Kanisa la Othodoksi, Walokole huko Marekani na Shirikisho la Kilimwengu la Makanisa

ya Matengenezo. Kuna uwezekano wa kuendelea kwa mwelekeo huu, na tunadumu kuona viongozi wa kanisa wengi zaidi wakisogezza madhehebu yao karibu zaidi na Rumi kupitia kauli na makubaliano ya pamoja. Biblia inasema kwamba hatimaye wote watakuwa katika upatanifu, watakuwa katika nia moja na mkakati mmoja, nao watampatia ‘mnyama’ (Kanisa Katoliki; Ufunuo 17:12-14) uwezo na mamlaka yao. Hivyo, leo tunaona utabiri wa Biblia kuhusu mwisho wa wakati ukitimia, mbele hasa ya macho yetu. Zaidi, kifupi, Biblia inasema kwamba tawala hizi zitampinga Kristo na wale walio upande Wake. Basi, katika wakati huu wa mapinduzi, tunalamika kuchagua njia yetu—je, tuwe upande wa Kristo, au pamoja na viongozi wa ulmwengu, ambao sasa wanaelekea upande tofauti?

Endapo Luther angekuwa hai na kuona jinsi makanisa ya Kilutheri “yalivyoshereheke” Matengenezo yake pamoja na Wakatoliki, angeweza kuwakaripia Wakatoliki na Waprotestanti walioasi. Hakika wale wanaoghilibiwa na Rumi ni Waprotestanti walioanguka. Ujumbe wa Biblia ni huu:



‘TOKENI kwake, enyi watu Wangu’ – Ufunuo 18:4.

Tunaona kwamba maneno ya Biblia yakitimizwa, kama vile, “Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule (utawala wa upapa), na “hao wafanya biashara wako walikuwa wakuu wa nchi, kwa kuwa mataifa yote walidanganywa kwa uchawi wako.” (Ufunuo 13:3 na 18:23). Upapa hutumia ushirikina, ambao ni werevu mkubwa kiasi kwamba wengi hawajui kabisa nini kinachofanyika. Lakini watakapokuwa wamefanikiwa kuwafanya wote wakubaliane na mkakati wao wa kimataifa na uundwaji wa sheria, hapo ndipo watawatesa wale wanaopingana nao na kudhihirisha mafundisho na mkakati wao dhalimu—kama tu walivyomtesa Luther, Hieronymus, Wycliffe, Hus, Berquin, Zwingli na wengine wengi..

Je, Kanisa Katoliki limebadilika?

Sasa miaka 500 baada ya Luther tunajiuliza: Hivi Kanisa Katoliki limebadilika? Hapana! Kanisa Katoliki huendelea kuhimiza mafundisho na mapokeo yasiyo ya Biblia. Hebu tuangalie machache mionganoni mwa hayo:

1 Hoja ya Kwanza:

Kanisa Katoliki huamini kwamba papa ni mwakilishi wa Yesu duniani. [Mwakilishi ni yule asimamaye badaya ya mwingine, kaimu.] Biblia kwa upande mwingine, inasema kwamba Yesu alimtuma Roho Mtakatifu ili achukue nafasi Yake. (Yohana 14:16-17). Wanaamini kwamba Petro alikuwa papa wa kwanza, lakini Petro mwenye mapungufu asingekuwa Mwakilishi wa Kristo. Yesu alisema: “*Juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu*” (Mathayo 16:15-18). Neno la



Picha: Fondazione Cariplo

Kiyunani la “mwamba huu” = Petra. Neno **Petra** humaanisha **mwamba**. Neno asilia la Kiyunani la jina Petro = Petros, ambalo humaanisha jiwe au jiwe libiringikalo. Ni juu ya Kristo ndipo tutajenga kanisa letu na wala si juu ya mtu mwenye udhaifu, kama vile ambavyo mapapa wote katika zama zote wamekuwa na mapungufu. Paulo anaandika kuhusiana na wana wa Israeli walipokuwa jangwani: “*Wote wakanywa kinywaji kile kile cha roho; kwa maana waliunywea mwamba wa roho uliowafuata; na mwamba ule ulikuwa ni Kristo.*” (1 Wakorintho 10:4). Yesu ndiye Mwamba huo na wala si Petro.

2 Hoja ya Pili:

Kanisa Katoliki huamini kwamba kasisi anapokuwa akigawa mkate wakati wa huduma ya Meza ya Bwana na kusema maneno kadhaa ya ajabu, wakati huo mkate hugeuka hasa na kuwa mwili halisi wa Yesu. Kwa namna hii wanatoa mwili

wa Yesu kama kafara mpya kila wakati wanaposhiriki kula mkate (katika huduma ya Meza ya Bwana). Wanaamini kwamba kasisi anaweza kumwumba Muumbaji na kisha wanamla. Yesu alipoanzisha huduma ya Meza ya Bwana, aliubariki mkate na kuumega akisema: "*Naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.*" (1 Wakorintho 11:24). Tunapokula mkate, hutukumbusha juu ya kafara ya Yesu kwa ajili ya pale kwenye msalaba wa Golgotha na kwamba mwili Wake ulivunjwa kwa ajili yetu na damu ilimwagwa kwa niaba yetu. Pamoja na hilo, Biblia inasema



kwamba Yesu alitolewa kafara mara moja tu (Waebrania 7:28; 9:28). Ni kitendo cha kumdhihaki Yesu na kafara Yake pale mwanadamu anapodai kumtoa upya kila wakati mkate unapoliwa na divai inaponyewa, kama ifanyikavyo katika huduma ya Meza ya Bwana katika Kanisa Katoliki. Hili huonesha tu kwamba hawakubali kafara ya Yesu kwamba toshelevu na hufaa kutuokoa..

3 Hoja ya Tatu:

Kanisa Katoliki limeondoa amri ya pili kutoka kwenye katekisimu yao. Amri ya pili inasema kwamba hatupaswi kuabudu sanamu za kuchonga. (Kutoka 20:4-6). Sanamu za Bikira Maria huabudiwa katika Kanisa Katoliki na waabudu huamini kwamba Mariamu ndiye aliyeonekana katika mji wa Fatima pamoja na maeneo mengine ulimwenguni. Mariamu, hata hivyo, alikufa takriban miaka 2000 iliyopita, kwa hiyo lazima hiyo ni roho nyingine inayojidihirisha kama Bikira Maria.

4 Hoja ya Nne:

Kanisa Katoliki huamini kwamba Bikira Maria alichukuliwa kwenda mbinguni na kwamba maombi yetu yanapaswa kupitia kwake kwanza, ili yaweze kumfikia Yesu na Baba. Hili ni jambo ambalo Wakatoliki wamejitungia wenyewe, kwa sababu Maria-mu alikufa takriba miaka 2000 iliyopita. Amelala kaburini, kama ilivyo kwa wengine wote ambao wamekufa na hungojea ufufuo. (1 Wathesalonike 4:15-17).

Biblia inasema wazi: '*Kwa maana wako watatu washuhudiao mbinguni, Baba, na Neno, na Roho Mtakatifu, na watatu hawa ni umoja.*' (I Yohana 5:7). Andiko hili limeondolewa katika Biblia nyingi za kisasa, kwa vile sababu mojawapo ni kwamba Kanisa Katoliki hutaka pawepo nafsi nne maalumu, watakatifu mbinguni, Mariamu akiwa ni wa nne, nao wanaelekeza maombi yao kwake. Lakini Yesu anasema: '*Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi*' (Yohana 14:6). Yesu ndiye mpatanishi pekee kati ya Baba na sisi. Maombi yetu humfikia Baba kupitia Yeye. "*Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu.*" (1 Timotheo 2:5).

5 Hoja ya Tano:

Kanisa Katoliki husema kwamba papa na makasisi wanaweza kusamehe dhambi. Swalii linaulizwa basi: Je, tumwendee kasisi, Mariamu au Yesu ili tuweze kupokea msamaha wa dhambi zetu? Biblia inaweka wazi "**dhambi ni uasi**" (1 Yohana 3:4). "**Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu**" (Warumi 3:23). "**Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti...**" (Warumi 6:23). Matokeo yake, mwanzoni sote tulihukumiwa kufa. Yesu ndiye pekee awezaye kutuokoa kutoka dhambini. Ametumba, alitupatia uhai Wake kwa ajili yetu na anaweza kutuweka huru kutoka katika hukumu ya dhambi. Yeye pekee ndiye ameishi maisha kamilifu bila dhambi hapa duniani. Tunasoma: "**Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi.**" (Waebrania 4:15). Kwa hiyo: "**Basi Mwana akiaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli.**" (Yohana 8:36).

Yesu pekee ndiye anayeweza kutuweka huru kama tukiungama na kutubu dhambi zetu na kumwomba msamaha.

Je, tumwendee kasisi, papa, au Yesu? Tayari tumeona kwamba kuna Mwokozi na Mpatanishi mmoja tu kati ya Mungu



Baba na sisi wanadamu—Yesu Kristo. Hatupaswi kusahau kwamba lazima tuungame makosa yetu kwa mtu ambaye tumemtendea dhambi. Tunasoma: "**Jilindeni; kama ndugu yako akikosa, mwonye; akitubu msamehe.**" (Luka 17:3).

Tutamwendea mtu ambaye tumemkosea, na kuungama dhambi yetu kisha kumruhusu mtu huyo atusamehe. Kasisi au papa hahusiki na suala hili. Hatimaye Yesu ndiye anayetusamehe. Tunasoma katika Sala ya Bwana: "**Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasameheyoye wadeni wetu.**" (Mathayo 6:12).

Yohana hulielezea hilo kwa namna hii:



"Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki." (1 Yohana 2:1-2).

Ni kupitia Yesu Kristo tu ndipo mdhambi anapoweza kusamehewa na hivyo kupewa fursa ya kuingia ufalme wa Mungu. Yesu pekee ndiye Mwokozi wetu, Mpatanishi wetu na Wakili wetu kwa Baba. Tunapaswa kwenda Kwake tukiwa na dhambi yetu.

Tunapotambua kuwa tumetenda dhambi, tumeungama na kutafuta msamaha, basi tunayo ahadi hii: “*Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.*” (1 Yohana 1:9).

Makasisi na papa wa Katoliki hujiweka katika nafasi ya Kristo na kujitwalia jukumu lake pale wanapodai kuwa na uwezo



wa kusamehe dhambi. Biblia imetabiri kwamba uasi huu ungetokea. Tunasoma: “*Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yo yote; maana hajji, usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu; yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu.*” (2 Wathesalonike 2:3-4).

Huyo aitwaye mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu na mpingamizi, hujiweka mahali pa Kristo. Anakaa katika hekalu la Mungu kana kwamba alikuwa Mungu. Si mwagine ila ni papa tunayemzungumzia. Ndiye mwasi ambaye amebadilisha Amri Kumi za Mungu. Huchukua nafasi ya Kristo kama mpatanishi na kusema anaweza kusamehe dhambi. Kwa nini ulimwengu wa Kiprotestanti ushirikiane na mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu, mpingamizi?

6 Hoja ya Sita:

Kanisa Katoliki huamini katika hali ya kutokufa kwa roho. Huamini kwamba mtu anapokufa, wanaenda kuishi katika namna ya nafsi au roho. Biblia inasemaje juu ya hili? Tunasoma: “*Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puanzi pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai.*” (Mwanzo 2:7). Inasema kwamba wanadamu *wakawa* nafsi hai na wala hawapokei roho. Tunasoma zaidi kuhusu kile hasa kinachokufa: “*Roho [nafsi] itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa.*” (Ezekieli 18:20).

Fundisho la kutokufa kwa roho mwanzo wake ni uongo wa kwanza wa Shetani katika Bustani ya Edeni. Mungu alimwambia Adamu na Hawa kwamba hawakupaswa kula matunda ya mti maalum bustanini. Kama wangekula matunda kutoka katika mti huu, wangekufa. Lakini Shetani alimwambia Hawa: Hapa, “*Hakika hamtakufa*” (Mwanzo 3:4).

Uongo huu kutoka kwa Shetani ndio msingi wa fundisho la kutokufa kwa roho na limeenea mionganoni mwa dini nyingi leo. Lakini Biblia inasemaje? Mwenye hekima Sulemani anasema: “*Kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lo lote, wala hawana ijara tena; maana kumbukumbu lao limesahauliwa. Mapenzi yao na machukio yao, na husuda yao, imepotea yote pamoja; wala hawana sehemu tena katika jambo lo lote lililofanyika chini ya jua... Lo lote mkono wako utakalolipata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako; kwa kuwa hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima, huko kuzimu uendako wewe.*” (Mhubiri 9:5-6, 10).

Hebu tuangalie maandiko mengine kadhaa zaidi: “*Msistaajabie maneno hayo; kwa*

maana saa yaja, ambayo watu wote walioomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu.” (Yohana 5:28, 29).

Paulo anafikia hitimisho hilo anapozungumzia Marejeo ya Pili ya Yesu: “*Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.*” (1 Wathesalonike 4:15-17).

Kwa hiyo tunaona kuwa wafu wamo makaburini na wataamshwa na Yesu. Je, hili linakushangaza? Tumeona kwamba wafu hawajui lolote. Wamelala kaburini hadi wakati wa ufufuo. Wenye haki wataamshwa kwa ajili ya ufufuo wa uzima na waovu kwa ajili ya ufufuo wa mauti.

Lazaro, rafiki wa Yesu, alipokuwa amekufa, Yesu alikuja kwake. Lazaro alikuwa amekufa siku nne kabla ya hapo na alikuwa ameanza kunuka. Yesu alisema kwamba Lazaro alikuwa amekufa na akalinganisha mauti na usingizi. Yesu alimwambia: “**Lazaro, njoo huku nje.**” (Yohana 11:43). Hakika Lazaro alitoka kaburini.

Wachungaji wengi wanahubiri kwamba, mtu anapokufa, anaenda mbinguni au jehanamu. Kama mtu mwenye haki anaenda moja kwa moja mbinguni anapokufa, basi tungepaswa kuamini kwamba Lazaro, rafiki wa Yesu, alikuwa ameenda mbinguni. Lakini hakushuka kutoka mbinguni, au au mawinguni au kutoka angani kwa vile Yesu alimfufua **Lazao kutoka kaburini.** Pia, Biblia inasema: “*Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu.*” (Waebrania 9:27). Hukumu itafanyika katika kipindi cha mauti na wakati wa kuja kwa Yesu mara ya pili na si kasisi, bali ni Yesu Kristo, atakayeamua wale watakaopokea uzima wa milele na wale watakaopokea hukumu ya milele. (2 Wakorintho 5:10; Yohana 5:26-29). Hakika Biblia inasema “*Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.*” (Warumi 6:23).



Katika kisa hiki tunajifunza pia kwamba Yesu atamfufua Lazaro katika siku ya mwisho. Martha alisema: “*Najua ya kuwa atafufuka katika ufufuo siku ya mwisho.*” (Yohana 11:24). Siku ya mwisho ni pale ambapo Yesu anakuja tena.

Biblia inasema kwamba ni Yesu pekee aliye na uwezo wa kutokufa au asiyepatikana na mauti. Imeandikwa: “*yeye aliye himidiwa, Mwenye uweza peke yake, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana; ambaye yeye peke yake hapatikani na mauti.*” (1 Timotheo 6:15-16). Mungu pekee ndiye hapatikani na mauti. Wanadamu wanakufa, lakini Yesu atakapokuja tena, wakati huo watavikwa kutokufa. Paulo hulieleza jambo hilo hivi: “*Angalieni, nawaambia ninyi siri; hatutalala sote, lakinisote tutabadijika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu,*

nasi tutabadijika. Maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa. Basi huu uharibikao utakapovaa kutokuharibika, na huu wa kufa utakapovaa kutokufa, hapo ndipo litakapokuwa lile neno lililoandikwa, Mauti imemezwa kwa kushinda.” (1 Wakorintho 15:51-54).

Wapo wengi wanaoamini kwamba ipo nafsi au roho inayoachwa huru pale mtu anapokufa na huwepo maeneo hayo ikishughulika na watu na ina uwezo wa kuwasiliana nao. Hii hapa nukuu kutoka katika gazeti la umizimu: “*Umizimu ninini? Umizimu ni imani kwamba roho inaendelea kuishi baada ya mwili kufa na inaweza kuwa na mawasiliano na watu walio hai kupitia watu tunaowaita wasihiri.*” (Imefasiliwa kutoka makala iitwayo Spiritisten, gazeti la Kidenmaki la umizimu, 1900, uk. 84).



Karibu nusu ya watu duniani huamini katika dhana ya kuzaliwa upya—fundisho linalosema kwamba roho haifi kamwe, lakini huzaliwa upya katika miili tofauti tangu kizazi hadi kizazi. Fundisho kama hilo halipatani na kile Biblia ifundishacho. Biblia inasema kwamba baada ya mauti, wanadamu wanakuwa mavumbi tena (Zaburi 104:29), wafu hawajui lolote (Mhubiri 9:5), hawana uwezo wa kiakili (Zaburi 146:4), hawashiriki katika lolote linalofanywa chini ya jua (Mhubiri 9:6), wafu hungojea kaburini (Ayubu 17:13), na wafu hawako hai (Ayubu 14:1, 2; 2 Wafalme 20:1).

Tayari tumeona kupitia maandiko mengi kwamba Biblia imejitenga kabisa mbali na nadharia ya kutokufa kwa roho, kuzaliwa upya kwa roho, umizimu na desturi za namna hiyo. Biblia huita mambo kama hayo machukizo. Tunasoma: ***"Asionekane mtu ampitishaye mwanawe au binti yake kati ya moto, wala asionekane mtu atazamaye bao, wala mtu atazamaye nyakati mbaya, wala mwenye kubashiri, wala msihiri, wala mtu alogaye kwa kupiga mafundo, wala mtu apandishaye pepo, wala mchawi, wala mtu awaombaye wafu. Kwa maana mtu atendaye hayo ni chukizo kwa Bwana; kisha ni kwa sababu ya hayo Bwana, Mungu wako, anawafukuza mbele yako."*** (Kumbukumbu 18:10-12).

Biblia hupinga kabisa mafundisho ya kutokufa kwa roho, umizimu, kuzaliwa upya kwa roho na falsafa/dini nyingine nyingi za siri huko mashariki.

7 Hoja ya Saba:

Kanisa Katoliki huwatisha watu kwa fundisho la mateso ya milele. Wamejaribu kuwashawishi watu kwamba wale ambao wamekataa kufuata mafundisho ya Katoliki



wataishia jehanamu. Wanasema kwamba kuna moto wa jehanamu uwakao milele na kwamba waovu wanaenda hapo na kuteswa kwa moto na kiberiti daima.

Kanisa liliuza vitubio. Walisema kwamba mtu angeweza kulipa fedha kanisani kama hakikisho kwa wangepewa adhabu ndogo wakati wa kufa wanapoenda pagatoria (toharani).

Wakati wa kipindi cha Matengenezo, pagatoria palieleweka kuwa mahali ambapo watu walikuwa wakiadhibiwa kwa ajili ya matendo yao mabaya kabla ya kuruhusiwa kuingia paradiso. Luther aliweka bayana kwamba fundisho kama hilo halikupatana kabisa na Biblia na lilitumiwa tu kuleta fedha kwenye masanduku ya Kanisa Katoliki.



Kanisa Katoliki hufundisha kwamba pagatoria ni eneo la kati kwa ajili ya adhabu ya muda kitambo pale mtu fulani anapokufa. Wale wanaoingia pagatoria hawawezi kutoka kwa uwezo wao wenyele lakini wanaweza kuwa na msaada kutoka kwa wengine. Kwa hiyo ndiyo sababu baadhi huwaombea wafu na hatu hulipa fedha kwa Kanisa Katoliki wakitumaini adhabu ndogo kwa wale walio pagatoria.

Papa pia alitoa msamaha kama njia ya kujipatia fedha. Hii inaitwa uuzaaji wa vitubio. Hebu tuelezee kidogo: Kama mtu alitenda dhambi, kwa mfano, uzinzi, au alivunja yoyote mionganoni mwa Amri Kumi, mtu huyo angeweza kujiepusha na adhabu ya kutenda dhambi hiyo kwa kulipa fedha. HUO ulikuwa msamaha wa dhambi. Wale walikuwa matajiri wangeweza kupata fursa ya kutenda dhambi nyingi.

Tetzel, aliyekuwa muuzaji wa vitubio na msemaji wa Kanisa Katoliki katika kipindi cha Luther, alitangaza kwamba kulingana na mamlaka ya barua ya vitubio, dhambi zote zilizotendwa na mnunuaji pamoja na dhambi yoyote itakayotendwa baadaye, ingesamehewa. Haikuwa muhimu kutubu kwa ajili ya dhambi. in. (D'Aubigne, kitabu cha 3, sura ya 1). Kwa namna hii watu walipokea uhakikisho kwamba vitubio hivi vingeweza kuleta wokovu si kwa walio hai tu, bali pia kwa wafu. Walidai kwamba mara tu baada ya fedha kulipwa, basi nafsi husika ingekuwa imelipiwa na kuondolewa pagatoria na hivyo ingepaa moja kwa moja hadi paradiso.

Katika zama zote watu wameyapatia makanisa fedha nyingi. Wengi wamelipa kiasi kikubwa cha fedha kwenda Kanisa Katoliki kwa sababu waliamini kwamba hilo lingesaidia wapendwa wao walikuwa katika mateso ya pagatoria. Kanisa Katoliki lilikuwa limetajirika kwa njia ya dhana za uongo. Kwa jinsi hiyo wamejilimbikizia kiasi kikubwa cha fedha katika nyakati zote kama matokeo ya propaganda zilizojengwa katika hofu. Wameweza kujenga makanisa/makathedro mengi mazuri kwa sababu ya udanganyifu na juhudhi hizi za kukusanya fedha. Wangepaswa kuona haya kwa namna walivyowadanganya watu.

Lakini Biblia inasema nini kuhusu kile kinachotokea pale watu wanapokufa? Biblia inasema kwamba **“mshahara wa dhambi ni mauti.”** (Warumi 6:23). Inaposema kwamba mshahara wa dhambi ni mauti, basi hakuna mateso baada ya hapo. Biblia inasema kwamba waovu

wanakabiliwa na adhabu yao kulingana na matendo yao. (Ufunuo 20:13). Endapo mtu fulani ametenda mambo mengi maovu, basi ataadhibiwa kwa muda mrefu na mateso makali zaidi. Nabii Malaki anathibitisha hili: ***“Kwa maana, angalieni, siku ile inakuja, inawaka kama tanuru; na watu wote wenye kiburi, nao wote watendao uovu, watakuwa makapi; na siku ile inayokuja itawateketeza, asema Bwana wa majeshi; hata haitawaachia shina wala tawi.”*** (Malaki 4:1). Shina au mzizi wa uovu wote ni Ibilisi na Shetani na matawi ni watu waovu. Wote watateketeza kama makapi. Majani mrefu na mabichi huwaka moto kwa muda mrefu, lakini majani mafupi na makavu huteketea kwa muda mfupi sana. Hii huonesha jinsi waovu watakavyoadhibiwa. Wataadhibiwa kulingana na matendo yao nao wataishia mautini. Lakini si wakati huu ndipo kuna adhabu katika ziwa la moto. Tunasoma kwamba ***“Kwa maana, angalieni, siku ile inakuja, inawaka kama tanuru”*** Hivyo hili litatokea wakati ujao, katika wakati wa mwisho.

Yohana anathibitisha hili anapoandika kuhusu waovu watakavyoadhibiwa katika ziwa la moto: ***“Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.”*** (Ufunuo 20:15). Mwandishi huyo anaelezea ziwa la moto katika namna hii: ***“Mauti na Kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili, yaani, hilo ziwa la moto.”*** (Ufunuo 20:14).

Yohana anaendelea kuandika: ***“Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji,***

na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili.” (Ufunuo 21:8).

Nini kilichowatoka waovu katika miji ya Sodoma na Gomora? Walichomwa kwa moto usiozimika, lakini hatimaye moto ulikoma mara baada ya kila kitu kuteketea. Biblia hulielezea kwa namna hii: ***“Kama vile Sodoma na Gomora na miji iliyokuwa kandokando, waliofuata uasherati kwa jinsi moja na hawa, wakaenda kufuata mambo ya mwili yasiyo ya asili, imewekwa kuwa dalili, wakiadhibiwa katika moto wa milele.”*** (Yuda 7). Andiko hili husema kwamba miji hii ilichomwa moto wa milele pamoja na wakazi wake. Ilikuwa adhabu kwa ajili ya udhalimu wao. Tunajua kuwa miji hii haiendelei kuteketea leo.



Moto ulikoma pale kile kitu kilipokuwa kimeteketea na kuwa majivu. Mtume Petro anaelezea kwamba hatima ya Sodoma na Gomora ni mfano wa kile kitakachotokea katika wakati wa mwisho. Anaandika: *“Tena akaihukumu miji ya Sodoma na Gomora, akiipindua na kuifanya majivu, akaifanya iwe ishara kwa watu watakaokuwa hawamchi Mungu baada ya haya.”* (2 Petro 2:6).

Adhabu itafanyika wakati ujao!

Yesu pia ametupatia neno Lake kuhusiana na suala hili kwa kusema: *“Basi, kama vile magugu yakusanyawyo na kuchomwa motoni; ndivo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia. Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi, na kuwatupa katika tanuru ya moto, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.”* (Mathayo 13:40-42).

Kwa mara nyingine tunaona hapa jinsi ambavyo adhabu itafanyika katika wakati ujao—mwishoni mwa wakati. Waovu hawaunguzwi katika jehanamu ya moto uwakao milele sasa, kama inavyofundishwa na Kanisa Katoliki. Fundisho hili la Katoliki

juu ya moto wa jehanamu ya milele kwa bahati mbaya imeenea hadi kwenye madhehebu ya Kiprotestanti!

Adhabu ya mwisho ya Shetani imeelezewa kwa namna hii: *“Kwa wingi wa maovu yako, katika uovu wa uchuuzi wako, umepatia unajisi patakatifu pako; basi nimetokeza moto kutoka ndani yako, nao umekuteketeza, nami nimekufanya kuwa majivu juu ya nchi, machoni pa watu wote wakutazamao. Wote wakujuao kati ya kabilia za watu watakustaajabia; umekuwa kitu cha kutisha, wala hutakuwapo tena hata milele.”* (Ezekiel 28:18-19).

Hakutakuwa na mateso ya milele kama ambavyo Kanisa Katoliko hufundisha. Adhabu ya waovu itaishia kwa mauti na majivu. Moto huo hauzimiki hadi adhabu inapokuwa imeisha na matokeo yake ni ya milele. Neno “milele” hutokana na neno la Kiyunani “aion,” lenye maana *ya muda mrefu, kipindi chote cha maisha, milele.* Hivyo waovu wanapoadhibiwa katika ziwa la moto *“muda mrefu”* au *“kipindi cha maisha yote”* kulingana na matendo yao, hii huishia katika mauti. Mungu ameahidi kukomesha kazi ya Ibilisi na pale waovu wote watakapokuwa wamekabiliana na adhabu yao, hapo ndipo Mungu ataumba mbingu na nchi mpya.

Mtume Petro anaandika juu ya hili: *“Lakini, kama ilivyio ahadi yake, mnatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake. Kwa hiyo, wapenzi, kwa kuwa mnatazamia mambo hayo, fanyeni bidii ili mwonekane katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake.”* (2 Petro 3:13-14). Yohana anafikia hitimisho hilohilo: *“Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena.”* (Ufunuo 21:1).



Tungependa kuuliza swali lifuatalo kwa wale wanaosisitiza katika kuamini mateso ya milele: “**Jehanamu iko wapi pale sayari dunia inapokuwa imeteketezwa na bahari ikiwa haipo tena?**” Haipo duniani kwa sababu chembechembe cha dunia zinateketezwa. Kila chembe ya uovu imetoweka. Hakuna chembe hata moja ya dhambi iliyosalia. Itaharibu tu uzoeufu mzuri wa wenye haki na hili Mungu ameliangalia mapema. Kwa hiyo uovu wote utateketezwa na kuharibiwa milele. Uovu wote unapokuwa umeondolewa, basi Mungu ataumba mbingu na nchi mpya. Kila kitu kitakachokuwepo ni amani na ustawi. Mungu ataanzisha upya kila kitu kama ilivyo kuwa katika Bustani ya Edeni kabla ya anguko, wakati ambapo mawasiliano na Mungu yalipofanyika ana kwa ana. Hapatakuwepo wezi, wala wasengenyaji, wala wauaji, wala askari, wala maumivu wala machozi katika nchi mpya. Biblia huielezea nchi mpya kama ifuatavyo: “**Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.**” (Ufunuo 21:4).

Kama ingelikuwa kwamba waovu wana-dumu katika mateso ya milele wasinge kuwa na mahali duniani kwa sababu hakuna tena maumivi, machozi, wala mateso hapo. Wenye haki wataishi katika nchi mpya. Hebu wote wanaosoma makala hii wamkubali Yesu Kristo na kuomba kwa ajili ya nguvu ya Roho Mtakatifu ili kuwa mashuhuda waaminifu na kuwa sehemu ya watu. Wake pale atakapowaita watu. Wake na kama matokeo yake kuwa sehemu ya wenye haki, ambao kwa neema ya Mungu, watairithi nchi mpya!

Nadharia ya mateso ya milele ni fundisho la kutisha lililojengwa katika hofu. Kwa hiyo litupwe motoni na kuliacha liteketee! Nadharia hii haihusiani kwa namna yoyote na upendo wa Yesu. Yesu anatamani tu mambo bora kwa ajili yetu Naye amemruhusu Shetani afanye kazi yake chafu ili wote waweze kuona kwamba yeze ni mwovu. Mungu hamlazimishi mtu yeyote. Lakini hili sivyo kwa Ibilisi. Ushahidi wote utakapowasilishwa, Mungu, kwa upendo, atamwangamiza Shetani na wale wote ambao wamejiunga naye katika kumwasi Mungu. Hivyo tunatazamia siku ya hukumu na wakati ambapo Mungu ataumba mbingu mpya na nchi mpya ambamo haki hukaa ndani yake na ambamo upendo wa Yesu hudumu pamoja na amani na furaha ya milele.

8 Hoja ya Nane:

Kanisa Katoliki hutekeleza na kufundisha ubatizo na kuwapatia kipaimara watoto wachanga. Ubatizo wa watoto wachanga chanzo chake ni fundisho la Augustine la dhambi ya asili. Aliamini kwamba mtoto alizaliwa akiwa na dhambi. Hivyo, endapo mtoto ni mgonjwa na angeweza kufa, ilikuwa lazima kumwomba kasisi aje haraka na kunyonyiza maji kichwani pa mtoto huyo. Hapo basi iliaminiwa kwamba mtoto huyo amekuwa Mkristo na kwamba amepata wokovu. Desturi hii inaendelea leo. Lakini mtoto mdogo hajafanya lolote baya. Haelewi jema na baya. Uwezo huu hukuzwa baadaye katika maisha yake. Biblia inasema kwamba “**dhambi ni uasi**” (1 Yohana 3:4) na kwamba “**Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa; mwana hatauchukua uovu wa baba yake.**” (Ezekieli 18:20).

Andiko hili linasema wazi kwamba mtoto harithi dhambi kutoka kwa wazazi wake.



Ni pale tu mtu anapokuwa mkubwa kiasi cha kuelewa tofauti kati ya jema na baya ndipo anaweza kuwajibika kwa ajili ya dhambi. Hivyo mtoto hana maisha ya kale ya dhambi yanayohitaji kuzikwa, kwa vile hana hatia hadi baadaye. Hivyo ubatizo wa watoto wadogo si muhimu na si fundisho la Biblia. Ukweli ni kwamba mtoto asiyejewa na hatia amekuja katika ulimwengu mwovu na amerithi asili ya dhambi ya wazazi wake na anashiriki hukumu ileile aliyopokea Adamu baada ya anguko: "***u mavumbi weve, nawe mavumbini utarudi.***" (Mwanzo 3:19). Licha ya hili mtoto mdogo hajakataa kazi ya ukombozi ambayo Kristo ameitenda kwa ajili ya wote. Wana fursa ya kupata ustahilifu Wake. Wakati ule akina mama walipowaleta watoto wao kwa Yesu, aliwaambia: "***Waacheni watoto wadogo waje kwangu, msiwazue; kwa maana watoto kama hawa usalme wa Mungu ni wao.... akawabarikia.***" (Marko 10:13-16). Yesu hakuwabatiza, lakini aliwabariki. Tunapaswa pia kulifanya hili mtoto awapo mdogo.

Nyuma ya fundisho la ubatizo wa watoto, wazazi-miungu ndio wanaopaswa kuamini kwa niaba ya watoto wao wadogo kwa vile mtoto hawezi kuamini. Lakini Biblia

inasema: "***Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.***" (Warumi 10:17). Mtoto mdogo haelewi hubiri/fundisho na hivyo hawezu kuwa na imani yake mwenyewe. Pia tunasoma: "***Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.***" (Marko 16:16). Matokeo yake, wale wanaotaka kubatizwa lazima wawe na imani binafsi. Hivyo ni makosa pale wazazi-miungu wanapotenda kwa niaba ya mtoto. Makasisi na wazazi-miungu wanasemwa kwamba mtoto atakuza imani yake mwenyewe baadaye wakati wa kipaimara, lakini hakuna uhakikisho wa hili.

Hebu tuangalie baadhi ya mifano ya ubatizo katika Biblia. Zingatia kwamba imani ni muhimu sana.

Filipo alipohubiri injili ya Yesu kwa towashi Mkushi, baadaye alimwambia Filipo: "***Tazama, maji haya; ni nini kinachonizua nisibatizwe? Filipo akasema, Ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana. Akajibu, akanena, Naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu. Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi; naye akambatiza.***" (Matendo 8:26-38).



Filipo alipohubiri injili huko Samaria, walikuwepo wengi waliokubali ujumbe huo. Biblia hutuambia juu ya matokeo ya mahubiri ya Filipo: “*Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake.*” (Matendo 8:12).

Wanaume na wanawake ndio waliobatizwa, si watoto.

Katika Biblia tunapata kisa juu ya mlinzi wa gereza aliyebatizwa pamoja na watu wa nyumba yake. Baadhi wanaweza kusema kwamba lazima walikuwepo watoto ambao pia walibatizwa. Hakuna dokezo kwamba walikuwepo watoto wadogo. Andiko linasema kwamba watu hawa walisikia kile kilichokuwa kinahubiriwa na wale walibatizwa walimpokea Yesu Kristo kwa Mwokozi wao binafsi. Tunasoma hapa juu ya kisa hiki: “*Kisha akawaleta nije akasema, Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka? Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako. Wakamwambia neno la Bwana, yeye na watu wote waliomo nyumbani mwake. Akawakaribisha saa ile ile ya usiku, akawaosha mapigo yao,*

kisha akabatizwa, yeye na watu wake wote wakati uo huo. Akawaleta juu nyumbani kwake, akawaandalia chakula, akafurahi sana, yeye na nyumba yake yote, maana amekwisha kumwamini Mungu.” (Matendo 16:30-34).

Hapa yupo Paulo akizungumza na mlinzi wa gereza huko Filipi na kwa watu wote wa nyumba yake. Walimpokea Yesu Kristo kwa imani nao walibatizwa. Kama walikuwepo watoto, wangepaswa kuwa wakubwa kwa vile Paulo aliweza kuwafundisha neno la Mungu.

Neno “ubatizo” hutokana na neno “baptismo” lililotumika katika shughuli ya sonara. Huelezajinsi kitu fulani kinapokuwa kimezama kabisa ndani ya maji. Endapo sonara aliposubu kipande cha chuma kwa namna fulani na endapo angetaka kibaki hivyo, basi angekitumbukiza kabisa kipande hicho cha chuma majini. Kupitia ubatizo, mtu husika huonesha kiishara kwamba ameikubali kafara ya Yesu, maziko na ufufuo Wake. Ubatizo pia huwakilisha kile ambacho kimefanyika ndani baada ya kuzika dhambi zote, kwa kuziweka kwa Yesu, ili aweze kuzipatanisha—kisha akiibuka na maisha mapya katika Kristo.



Hili hapa andiko la Biblia linaloelezea jambo hili: ***"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."*** (Warumi 6:3-4).

Andiko hili linasema wazi kwamba mtu ambaye amebatizwa amezikwa majini na huibuka katika maisha mapya katika Kristo. Hili si jambo linalofanyika katika ubatizo/ unyunyizaji wa watoto wadogo.

Biblia huita ubatizo “jibu la dhamiri safi mbele za Mungu” na husomeka kwa jinsi hii: ***“Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo.”*** (1 Petro 3:21).

Kama tungepaswa kufanya mapatano au kusaini mkataba na mtu fulani, ni muhimu sana kujua kile tunachokubaliana nacho kabla ya kusaini au kukubaliana na masharti hayo. Ndivyo ilivyo katika ubatizo. Kabla ya ubatizo, ni muhimu kutumia muda mwangi katika kujifunza Biblia na maombi ili kufahamu vigezo vya makubaliano/

agano. Hii ndiyo moja ya sababu inayofanywa ijulikane kama “ubatizo wa imani” au ubatizo wa watu wazima.” Kabla ya ubatizo, lazima tufanye maamuzi makini sana—uamuzi wa kumruhusu Mungu atubadilishe na kuomba uwezo wa kumfuata Yesu kila aendako. (1 Petro 2:21). Ubatizo hauna budi kuwa ishara ya nje ya badiliko ambalo tayari limefanyika ndani.

Huduma ya kipaimara ilianzishwa na Kanisa Katoliki katika karne ya 13. Uhalsia ni kwamba wachache tu wanaoshiriki katika kipaimara ndio humwamini Yesu Kristo kama Mwokozi wao binafsi. Hii huonesha kwamba desturi hii haitimizi kusudi lake. Martin Luther alitupilia mbali huduma ya kipaimara katika wakati wake na kuiita kile ambacho leo baadhi hutaja kama “matokeo ya ngedere ya mia moja.” Pia aliiona kama aina ya udanganyifu. Alimaanisha kwamba wote walitenda kama vile tu walivyotenda wengine wote na kupeana ahadi wao kwa wao, ambazo baada ya muda, wasingeweza kuzitimiza kabisa. Luther aliona kipaimara,



ambayo haikuungizwa Norway hadi mwaka 1736.

“Ubatizo” wa watoto wadogo na kipaimara ni mapokeo yaliyobuniwa na watu. Ni namna ya mbadala wa ubatizo wa Biblia. Hivyo ndivyo hasa Ibilisi atendavyo kazi. Anaweka uongo bandia mahali pa kweli ya Biblia, kitu fulani kinachofanana lakini hata hivyo ni tofauti.

Biblia inasema kwamba kuna **“Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja.”** (Waefeso 4:5). Tayari tumeona kwamba ubatizo wa kweli si ubatizo/ynyonyizo wa watoto wadogo, bali ubatizo wa imani, ambapo mtu anasikia injili na kufanya uamuzi binafsi wa kuukubali wokovu katika Yesu Kristo. Mtu husika, anayetazamia kubatizwa, anapaswa kufuata mfano wa Yesu. Yesu alibatizwa akiwa mtu mzima (umri wa miaka 30) katika Mto Yordani. Yesu hakuwa na haja ya kubatizwa kwa vile hakuwa na dhambi na hivyo hakuwa na haja ya wokovu. Licha ya hilo alibatizwa ili kutuachia kielelezo (Mathayo 3:13-17) ili tuweze kufuata nyayo Zake (1 Petro 2:21).

Tumesoma juu ya jinsi ambavyo katika ubatizo, mtu anazikwa majini na kuibuka katika maisha mapya katika Yesu. Hebu turejee kwenye historia na kufuatilia ubatizo wa Biblia na wala si ubatizo kulingana na Ukatoliki au Uprotestanti ulioasi. Ubatizo wa watoto wadogo na kipaimara ni mapokeo ya Kikatoliki na wale wanaoamini kwamba wataokolewa kwa vile wazazi wao walishiriki katika matendo haya pamoja nao, wamedanganywa. Hawajapitia ubatizo wa Biblia na hakuna aina nyingine ya ubatizo kulingana na Neno la Mungu. Wote wanaopenda kumfuata Yesu na kufanya kama alivyofanya watakubali kubatizwa kwa mujibu wa Biblia. Ubatizo wa watoto/ kunyonyiza si ubatizo wa Biblia. Wazazi



na wazazi-miungu ndio wanaoamini kwa niaba ya mtoto, lakini yule anayetarajia kubatizwa ndiye anayepaswa kuwa na imani yake mwenyewe. Yesu alimwambia Nikodemo: **“Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.”** (Yohana 3:5).

Yesu anasema kwamba hatuwezi kuja katika Ufalme wa Mungu kama tusipozaliwa kwa maji na kwa Roho. Hili linapaswa kutufunga jicho kila mmoja wetu!

Hebu sasa tushiriki katika ubatizo wa Yesu, ubatizo wa imani! Ubatizo wa wadogo/ynyonyizo si ubatizo. Ni mapokeo danganyifu yaliyovumbuliwa na mwana-damu!

9 Hoja ya Tisa:

Kanisa Katoliki husema kuna wokovu katika sakramenti mbalimbali—kama vile ubatizo, kushiriki katika Ekaristi, kufanya maungamo, nk. Luther alifundishwa pia mambo haya wakati akikua kama Mkatoliki. Siku moja wakati akitambaa kupanda ngazi, alikumbusha andiko lisemalo: **“Mwenye haki ataishi kwa imani”** (Warumi 1:17).



Hebu tuangalie baadhi ya maandiko yanayofafanua juu ya maana ya imani:

“Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajivayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.” (Waebrania 11:1).

“Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.” (Warumi 10:17).

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye.” (Yohana 3:16-17).

“Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema. Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu; ili katika zamani zinazokuja audhahirishe wingi wa neema yake upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo Yesu. Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asiye akajisifu. Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo.” (Waefeso 2:4-10).

“Aaminie na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.” (Marko 16:16).

Luther alisimama na kutambua kwamba alikuwa akitambaa ili kupata wokovu; alidhani matendo yangeweza kumwokoa. Hapo sasa aliangaziwa nuru akilini mwake. Alifikia hatua ya kuelewa kwamba ni kuitia imani tu katika Yesu Kristo, Mwokozi wa ulimwengu ndipo angeweza kuokolewa. Matendo hayawesi kutuokoa, lakini matendo ni matunda ya imani (Mathayo 5:8). Kadiri Luther alivyoendelea kujifunza mada hii, alipata maandiko kadhaa muhimu zaidi katika Neno la Mungu yaliyohusu kuwa na imani katika Yesu Kristo. Tunapokuja kwa Yesu jinsi tulivyo tukiwa na dhambi zetu zote, lazima tuziungame, tutubu na kumwomba msamaha. Hapo ndipo Yesu atasamehe dhambi zetu, na haki Yake itahesabiwa juu yetu, neema tusiyostahili itakuwa yetu kuitia imani. Hebu fikiria ni faraja ilioje ambayo lazima ilikuja maishani mwa Luther. Mimi na wewe tunaweza pia kupata uhuru huohuo, tunapofuata mpango wa Mungu.

Hivyo basi, matendo yana sehemu gani?

Tumesoma kwamba: “*Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo.*” (Waefeso 2:10).

Yohana Mbatizaji alipokuja na kuhubiri ujumbe wa uongofu, alisema: “**Basi zaeni matunda yapasayo toba.**” (Mathayo 3:8).

Yakobo anaandika: “*Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake.*” (Yakobo 2:17).

Hivyo imani pasipo matendo imekufa na matendo mema ni matunda ya imani.

Kwa imani, Habili alitoa kafara bora kuliko Kaini,

Kwa imani Nuhu alijenga safina,
Kwa imani walisafiri kuvuka Bahari ya Shamu,
Kwa imani wote watenda jambo fulani. Hii ni haki kwa imani.

Tunapoikubali haki ya Kristo, lazima pia tuombe ili kupata nguvu ya kuishi maisha ya haki kwa ajili Yake. Hapo ndipo tutakuwa mashuhuda Wake.

“**Kama mkijua ya kuwa yeye ni mwenye haki, jueni ya kuwa kila atendaye haki amezaliwa na yeye.**” (1 Yohana 2:29).

“**Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye; atendaye haki yuna haki, kama yeye alivyuo na haki;**” (1 Yohana 3:7).

Hivyo nguvu ya kuishi kwa uadilifu na kuzaa matunda haimo ndani yetu, bali hupatikana




Luther aktiwa na Ilani ya Kipapa aktiwasha moto wa Matengenezo.

katika uwezo wa Kristo ndani ya muumini. Paulo anatangaza: “*Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema.*” (Wafilipi 2:13).

Pamekuwepo mgogoro kati ya Kanisa Katoliki na Kanisa la Kilutheri tangu Luther alipojitekeza na kuhubiri haki kwa imani. Mnamo mwaka 1999, makanisa haya mawili kwa pamoja yameunda hati inayohusiana na haki kwa imani baada ya mijadala mingi, hatua nyingi za kidiplomasia na harakati za umoja wa makanisa. Hati hii inaitwa *Azimio la Pamoja (Joint Declaration)*. Azimio/ mapatano haya yalisainiwa mwezi Oktoba 31, 1999; miaka 482 kamili baada ya Luther kugongomelea hoja zake kwenye ukuta wa kanisa huko Wittenberg, ambapo alidokeza pia umuhimu wa haki kwa imani na kwa imani pekee. Hati hii, *Azimio la Pamoja*, lilirejesha Rumi Kanisa la Kilutheri, kwa vile linalezea kwamba kuna wokovu katika sakramenti.

Waprotestanti wameridhia, si Rumi

Sasa, miaka 500 baada ya Wittenberg, tunaona kwamba Wakatoliki na Waprotestanti wanamsherehekea Luther kwa pamoja.



Wanahafifisha hatua kubwa ya kujitenga kwa Luther kutoka Rumi na kusema kwamba sasa tuko katika zama mpya nasi tutasimama pamoja ili kuhamasisha **amanu** duniani. Lakini amani hii hutafutwa kwa harakati za umoja wa makanisa, diplomasia na kura ya wengi. Yesu alisema: “*Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike miyoni mwenu, wala msiwe na woga.*” (Yohana 14:27).

Amani ya kweli huja tu pale tunapompokea Yesu Kristo kama Bwana wetu katika maisha yetu, tunapokuwa tumeungama dhambi zetu na kupokea msamaha kutoka kwa Yesu, haki Yake, kwa neema kupitia imani. Uamuzi huu unapofanywa, hapo ndipo muumini atampokea Roho Mtakatifu kama chanzo cha nguvu katika maisha na hivyo atawea kuenenda katika hatua za Yesu—nguvu ya kutenda matendo mema.

Ulimwengu hauwezi kuleta amani hii halisi. Wale wanaochagua kufuata mikakati ya Rumi, inayoenda kinyume na mapenzi ya Mungu, hawatapokea amani hii ya ndani ambayo Yesu pekee ndiye awezaye kuitoa. Lazima tuchague kumkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wetu binafsi. Lazima tuchague kuwa watifi kwa Kristo—hapo ndipo nguvu yake itakuwa ndani yetu ili kufuata hatua Zake kupitia njia nyembamba.

- Wanamatengenezo walielewa maana ya kukubali wokovu katika Yesu Kristo. Hawakuwa wakielewa mambo yote lakini:
- Waanabaptisti walielewa maana ya ubatizo
 - Luther alielewa neema
 - Huss aliona maana ya utii
 - Wesley aliona umuhimu wa utakaso
 - Waldensia walielewa umuhimu wa Biblia
 - Miller alielewa maana ya marejeo ya pili ya Yesu

Habari gani sisi? Ndiyo, tumejifunza kidogo kuhusu kila moja ya mambo haya na hivyo tuna uelewa zaidi kuliko wale ambao wametutangulia. Lazima sasa tuangalie picha pana: Lazima sasa tuhubiri kweli hizi, ikiwa ni pamoja na imani, neema, wokovu, maisha ya Kristo, utendaji wa Roho Mtakatifu, ukuaji katika neema, ukuaji wa tabia, matunda ya Roho, Marejeo ya Pili ya Yesu na, mwisho, mada inayofuata..

10 Hoja ya Kumi:

Kanisa Katoliki limebadilisha Amri Kumi za Mungu. Kwa bahati mbaya, Luther alijumuisha amri za Kikatoliki kwenye katekisimu yake. Alikua kama Mkatoliki na hakutambua kosa lililofanywa na Kanisa Katoliki kuhusiana na Amri Kumi za Mungu.

Wameondoamri ya pili kwenye katekisimu na kugawa ile ya kumi mara mbili. Pia, wameondoamri sehemu ya amri ya nne. Pengine huu ndio udanganyifu mkuu zaidi katika historia ya ulimwengu. Licha ya hili, wapo wengi wanaoamini kwamba Kanisa Katoliki ni kanisa la Kikristo. Lakini Mkristo lazima amfuate Kristo na wala si kubadilisha chochote ambacho Kristo amesema au kuandika; tofauti na kile ambacho Kanisa Katoliki limefanya, na si tu kuhusiana na sheria ya Mungu. Kwa hiyo tunakubaliana na Luther na Wanamatengenezo, walioona vyema kwamba papa anabeba sifa za mpinga-Kristo.

Martin Luther huliweka kwa namna:

“Hapo awali nilisema kwamba papa alikuwa mwakilishi wa Kristo; sasa natangaza kwamba yeye ni adui mkuu wa Bwana wetu, mtume wa Ibilisi.”
(D'Aubigne, kitabu cha 7, sura ya 6).

Ilani ya kipapa ilipomfikia Luther, alisema: ***“Naidharau na kuishambulia, kuwa ni yenye kufuru na uongo.... Kristo Mwenyewe ndiye anayeshutumiwa humo.... Nafurahia kwa kustahimili maovu hayo kwa ajili ya faida ya kazi bora zaidi. Tayari najisikia kuwa na uhuru mkubwa zaidi moyoni mwangu; kwa vile hatimaye najua kwamba PAPA NI MPINGA-KRISTO, NA KWAMBA UTAWALA WAKE NI WA SHETANI MWENYEWE.”*** (D'Aubigne, kitabu cha 6, sura ya 9).

Ni Walutheri wangapi wasemao jambo hilo leo? Uliza kwa namna nytingine: Je, Kanisa la Kilutheri lenyewe kwa namna fulani ni mpingle-Kristo kwa vile limekubali Jumapili kama siku ya pumziko?

Kama ilivyodokezwa hapo awali, upapa umeondoamri mengi katika amri ya kwenye katekisimu yao.

Amri ya nne husema yafuatayo:


“Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivymo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.” (Kutoka 20:8-11).

Katika amri ya nne ya katekisimu, hakuna lolote linaloonesha kwamba Sabato ya siku ya saba ni siku halisi ya pumziko. Watu wengi wanafahamu vyema kwamba Yesu alikufa siku ya Ijumaa. Biblia huiita siku



Keeping the Lord's Day Holy

John Paul II



DIES DOMINI

CATHOLIC TRUTH SOCIETY

hii kuwa siku ya maandalio, siku kabla ya Sabato (Marko 15:42-43). Ni siku ya saba katika Biblia na ya mwisho katika juma. Kama ambavyo Yesu alipumzika kaburini, wanafunzi walikusanyika na kupumzika kama ilivyoamriwa (Luka 23:53-56). Siku inayofuata ilikuwa Jumapili. Jumapili ni siku ya kwanza ya juma katika Biblia. Katika siku hii Yesu alifufuka kutoka kwa wafu. (Marko 15:42-47; 16:1-6).

Wote wanaosoma maandiko haya wanaweza kuona vyema kwamba Jumapili ni siku ya kwanza ya juma katika Biblia na Sabato ni siku ya saba ya juma. Sabato ni siku ya Biblia ya pumziko. Wakristo wote wanapaswa kuiadhimisha siku ya Bwana Yesu ya pumziko kwa vile Yesu ndiye aliyeianzisha Sabato ya siku ya saba kama siku ya pumziko. Biblia inasema kwamba: “*Vyote vilifanyika kwa huyo.*” (Yohana 1:1-14). Biblia pia inasema kwamba **Yesu ni “Bwana wa Sabato.”** (Marko 2:27-28). Andiko hili hudhihirisha pia kwamba Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu. Wengi

huamini kwamba Sabato ilikusudiwa kwa ajili ya Wayahudi tu, kama ilivyoelezewa katika tanbihi za Biblia mpya ya umoja wa makanisa—Biblia ya Mwaka 2011. Lakini hili si kweli kwa vile tayari Sabato ilikuwa imeanzishwa tangu uumbaji. Tunasoma kwamba Mungu aliumba kwa siku sita na kupumzika katika siku ya saba. Hivyo tunaona kwamba Sabato asili yake ni katika uumbaji na wala si katika ufufuo wa Yesu. Siku ya ufufuo wa Kristo ni siku ya kwanza ya kazi ya juma baada ya Yesu kupumzika katika siku ya saba. Sivyo kwamba Yesu alikuwa na siku mbili za pumziko moja baada ya nyingine—siku ya 7 na siku ya 1 ya juma. Hapana, Yesu alipumzika kaburini katika Sabato na kufufuka katika siku mpya ya kazi Jumapili, siku ya kwanza ya juma, kama ambavyo, wakati wa uumbaji, alianza kuumba (kufanya kazi) katika siku ya kwanza ya juma.

Hakuna lolote katika Maandiko linalosema kwamba Yesu alituagiza kuacha kuishika Sabato ya siku ya saba na badala yake tuishike Jumapili, siku ya kwanza ya juma. Kama alikuwa amebadilisha hili, angefanua wazi jambo hilo. Pia angelazimika kubadilisha Amri Kumi, ambazo kwa namna bayana hutamka kwamba tunapaswa kuitunza Sabato ya siku ya saba kama siku yetu ya pumziko. Pia, Mungu habadiliki, kama ambavyo Biblia hubainisha wazi:

“Yesu Kristo ni yuleyule, jana, leo na milele.” (Waembrania 13:8).

“Kwa kuwa mimi, Bwana, sina kigeugeu...” (Malaki 3:6).

“Majani yakauka, ua lanyauka; Bali neno la Mungu wetu litasimama milele.” (Isaya 40:8).

Kanisa Katoliki hutamka kwa namna bayana kabisa kwamba walibadilisha siku ya pumziko. Tunasoma yafuatayo katika katekisimu ya Kanisa Katoliki:

Swali: Siku ya Sabato ni ipi?

Jibu: Jumamosi ni siku ya Sabato.

Swali: Kwa nini tunaadhimisha Jumapili badala ya Jumamosi?

Jibu: Tunaadhimisha Jumapili badala ya Jumamosi kwa sababu Kanisa Katoliki katika baraza la Laodikia (mwaka 336 B.K.) lilihamisha utakatifu kutoka Jumamosi hadi Jumapili.

Swali: Je, una namna nyingine yoyote ya kuthibitisha kwamba kanisa (Kanisa Katoliki) lina mamlaka ya kuanzisha sikukuu za sheria?

Jibu: Kama lisingekuwa na mamlaka hayo, lisingeweza kufanya hilo ambapo watu wote wa kidini wa sasa wanakubaliana nalo, lisingeweza kuweka uadhimishaji wa Jumapili, siku ya kwanza ya juma, mahali pa Jumamosi, siku ya saba, badiliko ambalo halina mamlaka ya kimaandiko.

Chanzo: “Doctrinal Catechism,” uk. 174 na “The Convert’s Catechism of Catholic Doctrine” (1977 edition), uk. 50.

Inavutia kugundua kwamba Sunday (Jumapili) humaanisha **“the day of the sun”** (**siku ya jua**) na wala si **“the Son’s day”** (**siku ya Mwana**). Mfalme Konstantine alikuwa wa kwanza kuanzisha Jumapili kama siku ya pumziko kwa sheria mnamo mwaka 321 B.K.: **“hebu mahakimu na watu wote wa mjini, na shughuli za biashara zote zipumzike katika siku ya jua yenye taadhima; lakini hebu wale walioko vijijini, kwa hiari na uhuru kamili**

wahudhurie katika shughuli ya kilimo.” - History of the Christian Church, 5 edition. volume 3, uk. 380.

Tunarudia, Jumapili (Sunday) inamaanisha siku ya jua (Day of the Sun), si siku ya Mwana (Son’s day).

Upotoshaji wa Agano

Ni dhahiri kabisa kwamba Kanisa Katoliki limefanya upotoshaji wa wasia au agano. Wasia au agano huandikwa pale mtu akiwa hai. Mtu anapokufa, agano hilo huwa halali na hakuna mtu yejote anayeweza kubadilisha maudhui ya agano hilo. Endapo mtu fulani akibadilisha wasia/agano, kwa namna hiyo linakuwa limepotoshwa. Hilo ndilo hasa ambalo Kanisa Katoliki limefanya. Wamepotosha hati kama hiyo kwa maana kwamba wamebadilisha Amri Kumi za Mungu na Sabato baada ya mauti ya Yesu. Tunaona kwamba wamefanya badiliko hili takriban miaka 300 baada ya kifo cha Yesu. Pengine huu ni udanganyifu mkuu zaidi wa hati katika historia na kosa hili limeandikwa katika vitabu vyta mbinguni.

Matokeo yake yana mvuto mkubwa. Mamiloni ya watu wamedanganyika kwa sababu ya upotoshaji huu. Tunawahurumia watu hawa kwa vile wamemtumainia kasisi/mchungaji na kuamini kwamba alihubiri kweli kutoka katika Neno la Mungu. Lakini sasa muda umewadia ili kufichua madanganyo na mateso ya Kanisa Katoliki ili wanaume na wanawake waweeze kujitenga mbali na mafundisho potofu yasiyo ya Biblia ya Kanisa Katoliki.

Papa Yohana Paulo wa II alikiri katika waraka wake wa kitume uitwao *Dies Domini*: **“Hii ndiyo sababu Wakristo, wakiwa kama watu walioitwa ili kutangaza uhuru uliopatikana kwa damu ya Kristo,**

walihisi kwamba walikuwa na mamlaka ya kuhamisha maana ya Sabato kuwa siku ya Ufufuo." (Dies Domini, pointi 63, ilichapishwa Mei 1998).

Pia aliandika: "*utajiri wa kiroho na kichungaji wa siku ya Jumapili, kama ilivyokabidhiwa kwetu kwa njia ya mapokeo.*"

Je, unaona madhaifu ya azimio la papa? Kwa uwazi kabisa papa anatambua kwamba uadhimishaji wa Sabato umebadilika kwenda katika uadhimishaji wa Jumapili. Kanisa Katoliki *lilihisi* kwamba lilikuwa na mamlaka ya kufanya badiliko hili. Hapa wanaweka mamlaka yao juu ya mamlaka ya Biblia. *Walihisi* kwamba walikuwa na mamlaka ya kufanya badiliko hili kuhusiana na siku ya pumziko.

Maamuzi mengi ya kushangaza yanaweza kuwa matokeo ya kufanya maamuzi yetu kulingana na hisia.

Papa pia anatambua kwamba Jumapili, kama siku ya pumziko, ni mapokeo. Kwa nini madhehebu mengine ya Kikristo hayawi wakweli kama Kanisa Katoliki na kuitambua Jumapili kama mapokeo? Ni kosa kabisa kwa Kanisa Katoliki kuhamisha maana ya Sabato kwenda katika siku ya ufufuo—jambo wasilokuwa na haki ya kufanya—lakini hata hivyo wanakiri kwamba wamefanya badiliko hili. Katika hukumu, haitajulikana tu kwamba tumeungama dhambi zetu, bali pia kwamba tumekuwa radhi kutubu na kuifuata njia ya Mungu.

Mwenye hekima Sulemani aliandika: "*Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu. Kwa maana Mungu ataleta*

hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya." (Mhubiri 12:13-14).

Hebu tuangalie nukuu mbili kutoka katika vyanzo vyta:

"Kanisa Katoliki kwa zaidi ya miaka elfu kabla ya uwepo wa Waprotestanti, kwa sababu ya utume wake wa kiungu libibadilisha siku husika kutoka Jumamosi kwenda Jumapili." (Catholic Mirror, Sept. 1893).

"Jumapili ni chapa yetu ya mamlaka. Kanisa liko juu ya Biblia, na badiliko hili la uadhimishaji wa Sabato (kwenda Jumapili) ni uthibitisho wa ukweli huo." (Catholic Record, London/Ontario, Sept. 1, 1923).

Hii hapa tena. Kanisa Katoliki linakiri kwamba wako juu ya Biblia. Wanasema kwamba wana mamlaka ya kiungu ya kubadili majira na sheria (Danieli 7:25). Wanajitwalia mamlaka yasiyopatana na Neno la Mungu.

Yesu alipojaribiwa na Ibilisi, alimrejesha katika Neno la Mungu. Alisema: "**“Imeandikwa”**" (Mathayo 4:10). Aliruhusu Maandiko yawe mamlaka Yake. Wale wasioruhusu Maandiko yawe mamlaka yao, hawana mamlaka kwa sababu mamlaka yako katika Neno la Mungu.

...lakini, hivi wanafunzi walibadilisha siku ya pumziko?

Baadhi husema kwamba wanafunzi walianza kuadhimisha Jumapili badala ya Jumamosi kama siku ya pumziko kama kumbukumbu ya ufufuo wa Yesu. Biblia iko kimya kabisa kuhusiana na badiliko hili. Baada ya kusoma rejea nane katika Biblia zinazohusiana na siku ya kwanza ya juma, hakuna hata amri au dokezo hata moja

linalowaonesha Wakristo wakiadhimisha Jumapili, siku ya kwanza ya juma, badala ya Jumamosi, siku ya saba ya juma. (Mathayo 28:1; Marko 16:2, 9; Luka 24:1; Yohana 20:1, 19; Matendo 20:7; 1 Kor. 16:2).

Kinyume chake, tunagundua katika Matendo kwamba wanafunzi waliendelea kuiadhimisha Sabato kama Yesu alivyo-kuwa amewafundisha. (Matendo 13:14-15; 13:42-44; 16:12-13; 17:1-2; 18:3-4)

Baraza la Trent

Baraza la kanisa lenye mamlaka makuu zaidi la Kanisa Katoliki lilikuwa Baraza la Trent (1545-63). Lengo lake kuu lilikuwa **“kubaini kwa namna mahususi mafundisho ya Kanisa katika kujibu uzushi wa Waprotestanti.”** – Catholic Encyclopedia, vol. XV, “The Council of Trent.”

Mamlaka yaliyojengwa katika mapokeo ya kanisa dhidi ya mamlaka ya Biblia yalifanyiwa mdahalo mzito katika baraza hili la kanisa. Uamuzi wa mwisho hatimaye ulifikasiwa katika kikao cha mwisho, ambapo huvutia kugundua kuwa hoja iliyodumu kwa mapokeo kushinda dhidi ya Biblia ilikuwa badiliko la Sabato (siku ya pumziko). Walihitimisha kwamba badiliko hili ulikuwa ushahidi wa mamlaka ya kanisa dhidi ya mamlaka ya Biblia. Hitimisho hilo linalelezewa kama ifuatavyo: **“Hatimaye... hali zote za kusita ziliwekwa pbeni. Askofu Mkuu wa Reggio alitoa hotuba ambapo alitangaza waziwazi kwamba mapokeo yalikuwa juu ya Maandiko. Hivyo, mamlaka ya kanisa yasingeweza kufungwa na mamlaka ya Maandiko, kwa sababu kanisa lilikuwa limebadilisha tohara kuwa ubatizo, Sabato kwenda**



Jumapili, si kwa amri ya Kristo, bali kwa mamlaka yake yenewe.” (J. H. Holtzman, Canon and Tradition, kilichochapishwa na Ludwigsburg, Germany, 1859, uk. 263).

Sasa tumefikia kiini cha suala husika. Waprotestanti na Wanamatengenezo walisema, na wanasesma leo, kwamba watayapokea Maandiko na Maandiko pekee kama msingi na mamlaka ya imani na mafundisho. Lakini upinzani wa Kanisa Katoliki dhidi ya Waprotestanti ni kwamba: Hapana, Waprotestanti hawana Maandiko pekee kama mamlaka yao kwa sababu wanashika siku ya kwanza ya juma, Jumapili, kama siku yao ya pumziko, wakati ambapo Biblia inasema wanapaswa kuishika siku ya saba, Jumamosi, kama siku ya pumziko. Tungepaswa kukubaliana na Wakatoliki katika suala hili. Wanakiri kwa unyofu kwamba walibadili siku ya pumziko kutoka Jumamosi kwenda Jumapili, siku ya saba ya juma kwenda siku ya kwanza ya juma. Wakati huohuo, wanawakemea Waprotestanti na Wanamatengenezo kwa sababu wanadai kuifuata Biblia, lakini kihalisia hawafanyi hivyo, kwa vile

wanafuata mapokeo ya Katoliki ya kushika siku ya kwanza ya juma kama siku yao ya pumziko.

“Kuna kimbilio moja tu lililobaki kwa Waprotestanti. Ni hilo ni kuchukua msimamo wao kwa uthabiti na kikamilifu katika ‘neno lililoandikwa tu’ Biblia na Biblia pekee. Waprotestanti hawajachelewa sana kiasi cha kufanya marekebisco. Je, watasanya hivyo? Je, watasimama kwa uthabiti na kufuata maungamo ya Kiprotestanti? Ama wataendelea bado kushikilia msimamo usioweza kutetewa, unaojipinga, na hatari sana wa kukiri kuwa Waprotestanti, lakini wakisimama katika viwanja vya Kikatoliki na kufuata mamlaka ya Kanisa Katoliki? Je, wataishika Sabato ya Bwana, siku ya saba, kulingana na Maandiko? Ama wataishika Jumapili kulingana na mapokeo ya Kanisa Katoliki” (Catholic Mirror, Sept. 2,9,16 & 23, 1893 vipeperushi vya Rome’s Challenge).

Rafiki mpendwa! Utachukua upande gani katika suala hili?

Martin Luther alithubutu kusimama na kuwa kinyume na kulikemea Kanisa Katoliki, alilojitenga nalo baadaye. Hakuwa na uelewa kamili wa sheria ya Mungu kwamba ilibadilishwa, ikiwa ni pamoja na badiliko la siku ya pumziko. Wale ambaao wangepaswa kufuata katika kazi yake ya matengenezo wangepaswa kwenda mbali zaidi hapo alipofika Luther, lakini badala yake wamerejea Rumi.

Waprotestanti wamekosea kuhusiana na suala la siku ya pumziko. Wamekubali mapokeo ya Katoliki na hivyo hawajafaalu katika kufikia lengo/kusudi la kufuata



Biblia na Biblia pekee kama mamlaka yao pekee ya imani na mafundisho. Taratibu Waprotestanti wamerejea Rumi kama matokeo ya uasi huu. Maridhiano haya na kuungana pamoja kutakumbukwa watakaposherehekea jubilii ya miaka 500 na kujitenga kwake na Kanisa Katoliki. Kuna umoja katika maana kwamba hakuna tena (isipokuwa wachache) Waprotestanti wa kweli, na Waprotestanti wa leo huifuata Biblia na mapokeo kama linavyofanya Kanisa Katoliki.

Sasa tunaweza kuangalia baadhi ya mapokeo yasiyo ya Biblia kutoka Rumi ambayo yamekubaliwa na Kanisa la Kilutheri pamoja na makanisa mengine mengi ya Kiprotestanti:

1. Karibu makanisa yote hufuata mapokeo ya utunzaji wa Jumapili, ambayo hayana misingi ya Biblia. Wanashika siku ya kwanza ya juma badala ya siku ya saba ya Biblia, Sabato.
2. Makanisa mengi hufuata mapokeo ya ubatizo wa watoto wadogo, ambayo hayana misingi ya Biblia, badala ya ubatizo wa imani.
3. Baadhi ya Makanisa hufuata mapokeo ya kipaimara ambapo vijana wenye umri wa miaka 13-14 huthibitisha imani, ambayo wao binafsi hawakuchagua “walipobatizwa” kama watoto wadogo.
Ni lipi onyo kali na la dhati kabisa ambalo Yesu huwapatia wale wanaowadanganya wengine? Yesu alisema: “Bali atakaye-

mkosesho mmojawapo wa wadogo hawa waniaminio, yamfaa afungiwe shingoni jiwe kubwa la kusagia, na kutoswa katika kilindi cha bahari. Ole ni wa ulimwengu kwa sababu ya mambo ya kukosesho! Maana hayana budi kuja mambo ya kukosesho; lakini ole wake mtu yule aliletaye jambo la kukosesho!” (Mathayo 18:6-7)..

Hitimisho

Matengenezo hayajafanikiwa katika kipindi kirefu, kwa sababu Biblia na Biblia pekee haijafuatwa. Ukweli kwamba wale wanaopaswa kuwa wawakilishi wa Matengenezo na Uprotestanti huishika Jumapili kama siku ya pumziko ni ushahidi bayana wa hili!

Wengi husema kwamba Matengenezo yaliishia kwa Luther, lakini lazima yaendelee hadi mwisho wa wakati. Luther alikuwa na jukumu kubwa la kutimiza katika kueneza nuru aliyopewa na Mungu. Lakini hakupokea nuru yote ambayo ulimwengu ungespaswa kupokea. Tangu wakati wake hadi sasa, kuna nuru mpya imebainika kwenye Maandiko na kweli mpya zimefunuliwa.

Nini kimetokea katika imani ya Biblia ya Wanamatengenezo? Leo tunalohitaji la mwanamatengenezo, kwa kweli, Wanamatengenezo wengi. Watu wanahitaji kuona mafundisho danganyifu katika makanisa mengi. Wakati huohuo, watu wanahitaji kusikia ujumbe bayana na wa kweli wa Biblia kwa ajili ya wakati wetu, kama tunavyopata katika Ufunuo sura ya 14, aya ya 6-12 na sura ya 18, aya ya mne. Nani atakayesimama kwa ajili ya kazi ya Mungu, kama ilivyokuwa kwa Luther jasiri?

Leo inaweza kuonekana kana kwamba tawala zote za ulimwengu zitashinda vita. Lakini Biblia hudhihirisha kwamba tawala hizi hupigana vita dhidi ya Kristo na wale walio katika upande Wake. (Ufunuo 17:12-14). Hili hutuonesha kwamba Mungu ndiye mwenye utawala na huweka mpaka. Ni wale walio upande Wake ndio watakaokuwa washindi katika vita kuu vya matengenezo, ambayo hudumu hadi mwisho hasa!

Kipimo kikubwa cha mwisho

Biblia hudhihirisha kwamba kipimo cha mwisho duniani, mara tu kabla ya Yesu Kristo, Mwokozi wa ulimwengu, kuja tena, kitakuwa kipimo juu ya ibada. Biblia huelezea kipimo hiki kama ifuatavyo: *“Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu ya mnyama, hata ile sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe. Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake.”* (Ufunuo 13:15-17).

Kwa hiyo kipimo kitakuwa ama tunamwabudu Mungu kama Muumbaji au tunamwabudu “mnyama” na kuipokea chapa yake. Tunarudia: Hili ni suala la ibada na wala siyo juu ya mikrochipu. Wengi huamini kwamba chapa ya mnyama ni mikrochipu. Mikrochipu pamoja na mfumo wa kielektroniki unawenza kutumika kama njia ya udhibiti katika kuwatawala wale wasiopokea chapa ya mnyama na hawataweza kununua na kuuza.

Fedha/pesa zote zitaondolewa na kadi au pesa za simu zitatumiwa. Mikro-chipu zitakuwa katika kadi au zinaweza kupandikizwa mwilini, ndani ya ngozi kwa mfano. Si tati zo kuzuia kadi au pesa ya simu fulani. Wale wasiopokea chapa ya mnyama wata-adhibiwa kwa sababu si watifi/waaminifu kwa tawala za kidunia. Adhabu yao itakuwa kushindwa kununua na kuuza. Ni mfano inaposemakwambachapayamnyama inaweza kupokelewa kwenye kipaji cha uso au mkononi. Kipaji cha uso huwakilisha ufahamu na mkono huwakilisha matendo au kazi. (Kumbukumbu 11:18). Tunafanya maamuzi na chaguzi katika sehemu ya mbele ya ubongo. Ama tunaweza kuchagua kukubalia chapa ya mnyama au tunaweza kuichagua kuititia matendo yetu. Biblia inasema kwamba tunapaswa kumwabudu Yeye aliyeumba mbingu na nchi. Amri ya nne hubainisha wazi nani tunayepaswa kumwabudu—Yeye aliyeumba katika siku sita na kupumzika katika siku ya saba. Ni kwa sababu siku ya pumziko inahusiana na ibada ndiyo maana hili litakuwa lengo mara kabl Yesu hajaja tena. Tunaishi katika wakati ambapo viongozi wa ulimwengu wanahimiza suala la Jumapili, siku ya kwanza ya juma katika Biblia, kama siku ya pumziko, siku ya familia na siku ya ibada. Huko Ulaya, The European Sunday Alliance inafanya jitihada za dhati katika kujaribu kuimarishe Jumapili kama siku ya



kila juma ya pumziko na siku ya familia. Huko Marekani, zipo harakati nyingi za kidini zilizoenea ambazo pia hutenda kazi ili kutimiza kusudi lilelile, kama The Christian Coalition na The Lord's Day Alliance, mionganoni mwa zingine.

Jumapili, kama siku ya pumziko, huenda kinyume na Neno la Mungu na Amri Kumi, ambapo iko wazi kuwa tutamwabudu Mungu katika siku aliyoitenga kama siku ya pumziko, Sabato, siku ya saba ya juma katika Biblia. Hivi karibuni ulimwengu utapimwa kuhusiana na ama utamwabudu Yeye aliyeumba mbingu na nchi na kutunza siku Yake ya pumziko, au ama watamwabudu “mnyama” (upapa) na kuiti na kuipokea chapa yake.

Tayari tumesoma baadhi ya nukuu kutoka Kanisa Katoliki ambako wanasema kwamba wana chapa. Wanasema kwamba chapa hii ni ishara ya mamlaka yao ya kubadili nyakati na sheria na kuanzisha mapokeo mapya kwa sababu walibadilisha siku ya pumziko. Biblia hudhihirisha kwamba hili ndilo hasa litakalotokea. Katika Danieli 7:25, inasema kwamba kanisa hili lingebadilisha nyakati na sheria.

Tayari tumeona kwamba wamebadili siku ya pumziko kutoka Sabato (Jumamosi) kwenda Jumapili. Sasa kwa vile umelitambua hili, ni mamlaka gani utakayokuwa aminifu kwayo au utakayoyatii?

Uchaguzi unaofanya utakuwa na matokeo uzima au mauti kwa sababu sasa umejulishwa kile ambacho kanisa lililoasi l i m e f a n y a k u h u s i a n a na siku ya p u m z i k o . Biblia inasema: “*Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi.*” (Yakobo 4:17).


Uamuzi huu ama kumwabudu Yeye aliyeumba au kumwabudu “mnyama na chapa yake” ni kitu fulani kinachofanyika katika wakati ujao. Hii itatokea wakati “chapa ya mnyama = uadhimishaji wa Jumapili ya kipapa” itakaposhurutishwa kwa sheria. (Ufunuo 13:15-16). Tunapaswa kufanya uamuzi leo kwa sababu hatujui tutaishi kwa muda mrefu zaidi kiasi gani. Leo ndiyo siku ya wokovu. “*Leo, kama mtaisikia sauti yake, Msifanye migumu mioyo yenu.*” (Waebrania 3:7-8).

Tunapofanya uchaguzi wa kumfuata Yesu leo, itakuwa rahisi zaidi kumfuata kesho!

Zingatia maandiko yafuatayo kwa uangalifu:

“*Mkinipenda, mtazishika amri zangu.*” (Yohana 14:15).

“*Katika hili twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu, tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake. Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si*



nzito.” (1 Yohana 5:2-3).

“*Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake. Lakini yeye alishikaye neno lake, katika huyo u p e n d o wa Mungu umekamilika kweli kweli. Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani yake.*” (1 Yohana 2:4-

5).

“*Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata.*” (Yohana 10:27).

Wito wa mwisho

Katika kuandika kuhusu madanganyo haya, tunaonya dhidi ya Kanisa Katoliki kama mfumo, ambao uko nyuma ya madanganyo na makosa mengi yanayohusiana na Neno la Mungu na hivyo hatuwahukumu Wakatoliki kama mtu mmojammoja. Ni mfumo wa Ukatoliki ndio tunaouzingatia na kuulinganisha na Neno la Mungu.

Hivyo tunatumaini kwamba maandishi haya yatawasaidia Wakatoliki na wengine wote wafikie hitimisho sahihi.

Tunaamini kwamba wapo watu waaminifu na wenye nia njema katika madhehebu mbalimbali, ikiwa ni pamoa na Kanisa Katoliki. Wengi watachukua msimamo dhidi ya madanganyo, ikiwa ni pamoa na lile la kubadili Amri Kumi, na

watajitenga na vifungo vinavyowashikilia katika makosa, wanapogundua mapokeo ya wanadamu ambayo yamejipenyeza katika makanisa mbalimbali. Tunaamini pia kwamba wale wanaotoka kwenye makanisa haya watakuwa mashahidi thabiti katika kuikamilisha kazi ya Mungu. Wito wa Biblia huwaenda watu wa Mungu walioko Babeli (Ukatoliki na Uprotestanti ulioasi): ***"Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake."*** (Ufunuo 18:4).

Kulingana na andiko hili, ni bayana kwamba wengi mionganoni mwa watu wa Mungu wako Babeli. Je, inawezekana kwamba wengi mionganoni mwa watu wa Mungu leo wanajikuta wakiwa Babeli? Wanapoona nuru kutoka katika Neno la Mungu na kutambua kwamba walidanganywa, kama ilivyokuwa kwa Martin Luther, watafuata wito wa Biblia wa kutoka Babeli na kuwa na neno la Mungu dhahiri kama mamlaka yao.

Kama uko ndani ya kanisa linalohamasisha/linalohubiri mafundisho haya yasiyo ya Biblia, ambayo tumeyagusia katika dondoo kumi, hebu toka kwenye kanisa hilo ili usije kukumbwa na hukumu ya waovu. (Ufunuo 21:8). Haifaidii kitu kuweka mguu mmoja Babeli na mwagine upande wa Mungu. Lazima tusimame miguu yote miwili ikiwa kamili upande wa Mungu. Je, unadhani kwamba utaokolewa kwa sababu u sehemu ya walio wengi? Biblia inasema kwamba watakuwepo masalia mwishoni mwa wakati—masalia ya wale wanaodai kuwa watu wa Mungu. Biblia huwaelezea masalia kwa maneno machache: ***"Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu."*** (Ufunuo 14:12)... si katika uwezo wetu, bali kwa uwezo wa Mungu katika

maisha yetu. (Wafilipi 2:13). Hawa ni masalia wa Mungu mwishoni mwa wakati. Wana nia moja, kama walivyokuwa wanafunzi wa Yesu wakati wa siku ya Pentekoste. Wana nia ya Kristo. (Wagalatia 5:22).

Hebu sote tuwe sehemu ya masalia hawa!

Salamu za kirafiki kutoka Abel na Bente Struksnes

Abel and Bente Struksnes

Vestrumsbygda 26, 2879 Odnes, Norway

www.endtime.net

Kwa maelezo zaidi juu ya mada hii na
mengine, endelea:

www.amazingfacts.org

www.amazingdiscoveries.org

www.greatcontroversy.net

www.KujifunzaBiblia.com

www.mwangaza.info

www.SwahiliTruth.org

GREGORIVS XIII·PONT·MAX

*Miaka 500
baada ya Luther:*

**Hoja 10 mpya
kwenye mlango
wa kanisa!**